


**NECTA** yaandaa mtihani kwa ajili ya waliofanya udanganyifu la VII

UKURASA 3





# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Desemba 11, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581156

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


UKURASA 9

# Mkutano wa CCM ulivyoacha maswali

UKURASA 2



Katibu Mkuu mstaafu wa CCM, Yusuf Makamba



Katibu Mkuu mstaafu wa CCM, Dk. Bashiru Ally.



Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan



Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### BILIONI 270/- KUTUMIKA MRADI WA SHULE BORA

SERIKALI ya Uingereza kupitia mfuko wa UK Aid imepanga kutumia Sh. bilioni 271 kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Shule Bora ambao utatekelezwa katika mikoa...

UKURASA WA 5

### UWT KUMSAIDIA RAIS SAMIA KUWAJIBIKA VIONGOZI WAZEMBE

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Mary Chatanda amesema hatasita kuwashughulikia wanawake viongozi, wakiwamo...

UKURASA WA 8

### TANZANIA YAISHUKURU KOREA KUTENGA MKOPO WA MABILIONI

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ameishukuru Serikali ya Jamhuri ya Korea kwa kutenga dola za Marekani bilioni moja zitakazotolewa kwa njia ya...

# Wabaini hujuma Daraja la Magufuli

UKURASA 3



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Wilbroad Mutafungwa (wa pili kushoto), akionyesha kwa waandishi wa habari jana, vifaa vya ujenzi wa daraja la Kigongo-Busisi maarufu Daraja la JPM, vilivyokamatwa baada ya kuibwa na baadhi ya wafanyakazi wa ujenzi wa daraja hilo, kwa kushirikiana na watu wengine. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Ramani ya mauaji ya trafiki yawasilishwa mahakamani

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA KAZI MOJA KWA KURUGENZI LEO UK.24

**KATUNI** UK.6



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe (kushoto), akimpongeza Rais wa tano wa Ukraine, Petro Poroshenko (katikati), baada ya yeye na Waziri Mkuu wa zamani wa nchi hiyo, Yulia Tymoshenko (hayupo pichani), kutangazwa kuwa washindi wa tuzo ya Bush-Thatcher 2022, kwa kupigania uhuru wa nchi yao, inayotolewa na Umoja wa Vyama vya Kidemokrasia Duniani (IDU), wakati wa kilele cha mkutano wa IDU, jijini Washington DC, Marekani mwishoni mwa wiki. Tuzo hiyo, iliwahi kutolewa kwa Chadema mwaka 2020. Kulia ni Mwenyekiti wa IDU na Waziri Mkuu mstaafu wa Canada, Stephen Harper. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkutano mkuu CCM ulivyoacha maswali

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) wiki hii kilifanya Mkutano Mkuu wa Taifa wa 10 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete (JKCC) jijini Dodoma. Mkutano huo uliofanyika Desemba 7 na 8 chini ya Mwenyekiti wake, Rais Samia Suluhu Hassan, ulikuwa wa kikatiba na hufanyika kila baada ya miaka mitano.

Mkutano Mkuu huo ambao pamoja na mambo mengine uliwachagua mwenyekiti wa taifa, makamu wenyeviti bara na Zanzibar na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) kutoka makundi ya wanawake na wanaume pande zote.

Rais Samia alichaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa CCM huku Abdulrahman Kinana akiendelea kuaminiwa katika nafasi ya Makamu Mwenyekiti Bara na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyetiki Zanzibar.

Licha ya viongozi hao wakuu wa chama kuchaguliwa, mkutano huo mkuu umeacha maswali mengi ambayo yanashindwa kutoa majawabu ya moja kwa moja huku wateule ndani ya chama na serikali wakiwekwa njiapanda kuhusu uhakika wa kuendelea kutumika katika nafasi walizo nazo.

**KIPORO MABADILIKO**

Kama ilivyo ada unapofanyika mkutano mkuu wa Taifa, mabadiliko makubwa hutarajiwa hasa katika sekretarieti kwa maana ya Katibu Mkuu na naibu makatibu wakuu wa Bara na Zanzibar, wakuu wa idara za fedha na uchumi, itikadi na uenezi, organaizesheni, na siasa na uhusiano wa kimataifa.

Tofauti na ilivyozoeleka, mabadiliko ya sekretarieti hiyo yamewekwa kiporo huku ikiahidiwa kuwa yatafanyika siku chache zijazo. Sekretarieti hiyo huteuliwa na NEC, hivyo majaliwa ya vigogo walioko katika nafasi hizo yako mikononi mwa wajumbe wa chombo hicho ambacho ni kama bunge la chama.

Kutokana na hali hiyo, wajumbe wa sekretarieti, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Daniel Chongolo, presha inapanda, mara inashuka kwa kuwa hawaelewi mustakabali wao kama wataendelea au la. Miongoni mwao waligombea ujumbe wa NEC huku baadhi wakipeta na wengine kuangukia pua.

**SERIKALI KUFUMULIWA**

Katika hotuba yake ya kufunga mkutano huo, Mwenyekiti wa Taifa wa CCM, Rais Samia, aliomba wajumbe wa Mkutano Mkuu wampe ridhaa ya kuifumua serikali yake kwa kile alichoeleza kuwa kuna baadhi ya wateule wake hawaendani na kasi yake.

Hali hiyo inazua maswali ni mabadiliko gani yatatokea kwa azma ya Rais Samia kuifumua serikali kama alivyoomba. Azma hiyo haijabainisha ni eneo gani ambalo anakusudia kufumua, hivyo kuwafanya wateule wake kuwa katika hali ya wasiwasi.

Iwapo atadhamiria kweli kufanya mabadiliko makubwa kwa kile alichosema ni kuifumua serikali, maana yake ni kwamba mawaziri na naibu mawaziri, makatibu wakuu na naibu makatibu wakuu, wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa mikoa na wakurugenzi wa halmashauri wako katika hofu kubwa ya kukumbwa na fumuafumua hiyo.

Mbali na wateule hao kuwa katika hali ya hofu, wananchi nao wako katika taharuki ya kutaka kujua ni mkeka gani wa wateule utaanza kutolewa na upi utafuata.

Pia wananchi hao na hata wateule wanajiuliza swali ambalo halina majibu ya moja kwa moja kwamba je, itafika Krismasi na Mwaka Mpya bila kuwapo mabadiliko?

Aidha, kutokana na taarifa hiyo ya kufumuliwa kwa serikali, baadhi ya wateule kwa maana ya mawaziri na manaibu wao, makatibu wakuu na manaibu wao, wakuu wa mikoa na wilaya, na wakurugenzi wa halmashauri, wameingiwa na hofu huku miongoni mwao wakisherehekea sikukuu za mwisho na mwanzo wa mwaka kwa hofu kama wataendelea kuwapo katika timu ya Samia au watatupwa nje.

**MBIO URAIS 2025**

Kwa muda mrefu tangu Rais Samia aingie madarakani na baadaye kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Taifa, kumekuwa na maneno na minong'ono kuwa kuna kundi ambalo linajiandaa kumpinga katika kinyang'anyiro cha urais ndani ya chama hicho mwaka 2025.

Licha ya minong'ono hiyo na taarifa kusambaa kwenye mitandao ya kijamii, Rais Samia mwenyewe aliwahi kusema kuna watu ndani ya serikali yake wana mipango ya kuwania urais, hivyo akasema ni vyema awaondoe katika safu yake ya uongozi ili wakajiandae vizuri badala ya kuwa nao na matokeo yake wakamhujumu katika jitihada za kuwaletea wananchi maendeleo.

Jambo hilo alilitimiza mapema mwaka huu alipofanya mabadiliko makubwa katika Baraza la Mawaziri kwa kuwacha baadhi ya wakongwe waliokuwamo katika awamu zilizopita na ambao walikuwa katika nafasi nyeti.

Mbali na kutekeleza hilo, wakati wa mkutano mkuu uliomalizika majuzi, Rais mstaafu na Mwenyekiti mstaafu wa CCM, Jakaya Kikwete, Dk. Ali Mohamed Shein, na katibu Mkuu mstaafu wa CCM, Mzee Yussuf Makamba, walitoa kauli ambazo zilionyesha kwamba ndani ya chama mambo si shwari hususan mbio kuelekea mwaka 2025.

Viongozi hao bila kuuma maneno, walikemea vikali juu ya watu wanaomendea urais mwaka 2025 na kusisitiza kuwa kama kuna mtu au kikundi cha watu ndani ya CCM waachane na mpango huo. Zaidi ya hapo, walisema wazi kuwa hakuna mtu ndani ya CCM wa kumpinga Rais Samia utakapofika wakati huo.

**KAULI ZA WAZEE**

Mbali na mbio za urais ndani ya CCM mwaka 2025, kumekuwa na baadhi ya watu ndani ya chama hicho wanaopinga jitihada za Rais Samia ikiwamo kumkosoa kupitia mitandao ya kijamii na kuleta maneno ya uchochezi.

Hali hiyo iliwaibua wazee, Kikwete, Mzee Makamba na Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ambao walitoa kauli nzito dhidi ya watu hao ambao walielezwa kuwa ni watovu wa maadili, hivyo wanapaswa kushughulikiwa na ikiwezekana wachukuliwe hatua kali ikiwamo kufukuzwa uanachama. Kauli hizo za wazee zimeibua maswali ikiwamo, je wanaodaiwa kumpinga Rais Samia ikiwamo katika kinyang'anyiro cha urais mwaka 2025 wataitwa na kamati ya maadili ya chama na kuchukuliwa hatua?

**ANGUKO LA VIGOGO**

Uchaguzi wa wajumbe wa NEC kwenye Mkutano Mkuu wa CCM, umewaacha baadhi ya wadau wa siasa na maswali yasiyo na majibu. Hiyo ni kutokana na baadhi ya vigogo na wakongwe ndani ya chama na serikali kuangukia pua.

Miongoni mwa walioanguka ni mawaziri na naibu mawaziri walioko ndani ya serikali, mawaziri wa zamani na wakuu wa idara za sekretarieti ya CCM. Anguko hilo linaibua swali, je, mwisho wao wa kisiasa umekaribia?


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

BELIA JOHN MWIGURA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA RACTIS** yenye usajili namba **T 570 DCG**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **KW/RB/5644/2022**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

MARIA IRENE TUTAH anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAUM** yenye usajili namba **T 758 DKF**, CHASSIS NAMBA: **NCZ200047239** na ENGINE NAMBA: **1NZB167359**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DSM/PHQ/RB/463799/2022.**


# Mahakama yapokea ramani mauaji trafiki

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imepokea ramani ya tukio la mauaji ya askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Sajenti Mensah aliyeuawa akiwa kazini eneo la mataa ya Sayansi, Kijitonyama Julai 22, 2016 kama kielelezo katika kesi hiyo.

Kijana Amani Filipo anatuhumiwa kumuua Sajenti Mensah kwa kumpiga risasi baada ya kumvamia katika kibanda cha polisi cha kupumzikia kilichoko mataa ya Sayansi kwa lengo la kutaka kupora.

Kielelezo hicho kilipokewa juzi na Hakimu Mkazi Mkuu, Romuli Mbuya wa Mahakama hiyo baada ya shahidi namba tano, askari polisi Hassan Luto kuiomba Mahakama ikipokee kama kielelezo.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Yasinta Lyimo, Luto ambaye ni mpelelezi wa kesi hiyo, alidai kuwa Julai 23, 2016, alikuwa kazini akiendelea na majukumu yake ya kazi.

Alidai kuwa aliitwa na mkubwa wa kazi yeye na wenzake wawili; Sajenti Bisima na Sajenti Ndege, wakipewa jalada la mauaji ya Sajenti Mensah kwa ajili ya upelelezi na walikwenda eneo la tukio.

"Tulikuwa tunalifahamu eneo hilo, lakini tulikuwa tukiongozwa na askari Ashirafu ambaye siku ya tukio alikuwapo, kwa hiyo alichora ramani ya tukio hilo na kuhoji mashahidi mbalimbali katika eneo hilo," alidai.

Luto alidai kuwa ramani hiyo aliyoichora ilionyesha Sajenti Mensah pamoja na shemeji yake wakati tukio linatokea walikuwa wamesimama, shemeji yake akiwa nje ya kibanda hicho.

"Ninaitambua ramani hii kwa sababu niliichora na nimeweza kuitambua kwa sababu ya mwandiko wangu na sahihi yangu, ninaiomba mahakama ipokee kama kielelezo katika kesi hii," aliomba Luto.

Hakimu Mbuya alikubaliana na ombi hilo, akapokea kielelezo hicho, ambapo upande wa mashtaka umefunga ushahidi wa mashahidi sita na mshtakiwa Amani ataanza kujitetea kesho.

Luto akijibu maswali ya Wakili wa mshtakiwa, Hassan Kiangio alidai eneo la Kijitonyama lina benki, lakini si benki zote zinalindwa na askari polisi.

## HABARI KITAIFA

# NECTA yaja na mtihani mpya darasa la VII

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Mitihani (NECTA) limetoa fursa kwa watahiniwa 2,194 waliofutiwa matokeo ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) mwaka huu, kufanya mtihani wa marudio utakaofanyika kwa siku mbili kuanzia Desemba 21 baada ya wadau kulalamika.

Katika mtihani huo uliofanyika kwa siku mbili kuanzia Oktoba 5 mwaka huu na matokeo yake kutangazwa Desemba Mosi, watahiniwa hao sawa na asilimia 0.16 ya watahiniwa 1,350,881 walibainika kufanya udanganyifu. Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Kaimu Katibu Mtendaji wa NECTA, Athumani Amasi alisema baada ya matokeo hayo kutangazwa, baraza limeendelea kupokea malalamiko kutoka kwa wadau wakiwamo wazazi na walezi.

Amasi alisema wadau wamelalamika kuwa udanganyifu uliofanyika katika mtihani huo, ulipangwa na kutekelezwa na uongozi wa shule husika, walimu na wasimamizi wa mtihani ambao waliwapatia watahiniwa majibu ya mtihani. "Wadau wamelalamika kwa kuzingatia umri wa watoto waliofutiwa matokeo, wasingeweza kuyakataa majibu waliyopewa na walimu au wasimamizi wa mtihani.

"Baraza limetafakari kwa kina malalamiko ya wadau na kuona kuwa ni ya msingi, hivyo limeamua kuwapa fursa watahiniwa 2,194 waliofutiwa matokeo, kufanya mtihani wa marudio mapema badala ya kusubiri hadi mwakani," alisema. Amasi alisema mtihani wa marudio umepangwa kufanyika kwa siku mbili kuanzia Desemba 21 mwaka huu.

Alisema kwa watahiniwa ambao shule zao zimefungiwa kuwa vituo vya mtihani, watafanyia mtihani wao kwenye vituo vya jirani na shule zao na wale ambao hawakufungiwa watafanyia shuleni kwao.

"Mtihani huu wa marudio utaendeshwa na kusimamiwa na Kamati za Uendeshaji Mitihani za mikoa husika kwa kuzingatia kanuni na taratibu za uendeshaji wa mitihani ya taifa," alisema.

Aliongeza kuwa matokeo ya watahiniwa watakaorudia mtihani yatawasilishwa mapema kwenye mamlaka zinazohusika na uteuzi wa wanafunzi watakaojiunga na kidato cha kwanza mwakani, ili waanze masomo pamoja na wenzao. Alipoulizwa kama utaratibu huo ndiyo utakuwa mpya ndani ya baraza, Amasi alisema hawatagemei tena shule kufanya udanganyifu kama wa mwaka huu. Alisema katika matokeo ya mtihani huo, baraza lilivifungia vituo vya mtihani 24 sawa na asilimia 0.13 ya vituo 17,935 vya mitihani vilivyothibitika kupanga na kufanya udanganyifu katika mtihani huo.

Alivitaja vituo 24 vilivyofungiwa na vituo vipya mbadala vitakavyotumika kwenye mtihani huo kwenye mabano kuwa ni High Challenge (Arusha), Kilimanjaro (Arusha, Arumeru), Al-Hikma (Sandali, Dar es Salaam), St. Anne Marie (Temboni, Ubungo), Kadama (Maweni, Chato) na Jamia (Nshambya, Manispaa ya Bukoba).

Vingine ni Karume (Nshambya, Manispaa ya Bukoba), Kazoba (Kambarage, Karagwe), Rweikiza (Nshambya, Manispaa ya Bukoba), Leaders (Mika, Rorya), St. Severine (Rubondo, Biharamulo) na Moregas (Turwa, Tarime). Vituo vingine ni Busara, Kivulini na Mugini ambavyo watahiniwa wake watafanya mtihani wa marudio kwenye kituo cha Magu mkoani Mwanza; Musabe na Olele watafanyia kituo cha Buhongwa jijini Mwanza.

Vingine ni Peaceland (Bukongo, Ukerewe), Tumaini (Kilabela, Sengerema), Ukerewe (Bukongo, Ukerewe), Winners (Buhongwa, Mwanza Jiji), Mustlead (Masuguru, Chalinze), Elisabene (Maporomoko, Tunduma) na Sahere (Bombo, Tanga Jiji)," alisema.

## Polisi wabaini hujuma kwenye Daraja la JPM

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limekamata vifaa mbalimbali vilivyoibiwa kwenye mradi wa ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi, maarufu Daraja la JPM.

Vilevile, jeshi hilo linamshikilia mlinzi wa Kampuni ya Ulinzi ya Cops Security Tanzania, Bwire Manyama kwa tuhuma za kushirikiana na wezi hao kuiba vifaa hivyo kwa kutumia mitumbwi ya wavuvi.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi Wilbroad Mutafungwa alisema jana kuwa tukio hilo la wizi linahusisha pia baadhi ya wafanyakazi wa mradi huo. Kamanda Mutafungwa alisema kuwa Alhamisi ya wiki hii, majira ya saa 1:30 asubuhi, Jeshi la Polisi lilipokea taarifa kutoka kwa kampuni ya ujenzi wa daraja hilo ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC), kuhusu wizi huo. Alisema kupitia taarifa za kiintelijensia walifika katika Kitongoji cha Busisi Madukani kwenye nyumba inayomilikiwa na Makona Samwel na kukuta vitu mbalimbali vikiwa vimefichwa huko.

"Upekuzi uliofanywa katika chumba cha Halfani Seif ambaye ni mfanyakazi wa kampuni ya CCECC kama fundi nondo, tulifanikiwa kuvikuta vifaa vyote vilivyoibiwa katika mradi," alisema.

Kamanda Mutafungwa alivitaja vifaa hivyo vilivyokuwa vimeibwa ni pamoja na mashine saba za kuchomelea, stick za kuchomelea vyuma aina ya THJ 422 maboksi 30, welding cable na drilling bit mbili, vyote thamani yake haijafahamika.

Alidai uchunguzi wa awali umeonyesha wezi hao walishirikiana na mfanyakazi wa kampuni ya CCECC, Humphrey William ambaye ni fundi wa kuchomelea pamoja na mlinzi Manyama.

Alisema kwa sasa wanamshikilia Bwire pamoja na gari lenye namba za usajili T 707 BPG aina ya Toyota NOAH, rangi nyeusi, linalodaiwa kuhusika katika kubeba vifaa hivyo siku ya tukio.

Kamanda Mutafungwa alisema gari hilo lilikutwa limetelekezwa eneo la Busisi Madukani wilayani Sengerema.

Ofisa Utawala wa kampuni ya CCECC, Yang Neng aliiomba serikali kuendelea kuimarisha ulinzi na kufanya msako wa mara kwa mara katika daraja hilo ili kudhibiti vitendo vya wizi vinavyorudisha nyuma mwenendo wa ujenzi wa daraja hilo.

IGT INSURANCE Co.

**DEATH ANNOUNCEMENT**

It is with deep regret and sadness that the Shareholders, Board of Directors, Management and Staff of Insurance Group of Tanzania Ltd regret to inform you that our Shareholder and Former Chairman **Ambassador Abubaker Rajab Ibrahim** has passed away on 7th December 2022 in India.

We wish his family and friends strength and guidance in this difficult time and may they know that we are with them. May the Almighty God give them strength to overcome this great grief.

Funeral Arrangements are underway at his Moshi residency and the burial will be conducted at Moshi Municipality, Kilimanjaro.

May his soul rest in peace.

**Victor Malewo**
**BOARD CHAIRMAN**



17190202

RIPOTI MAALUM-2

# Familia zinavyogeuza watoto kitega uchumi kupitia ukahaba

## ■Ustawi wa Jamii, wanasheria watoa tahadhari

Na Halfani Chusi

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana ilikuwa na ushuhuda wa binti anayetumikishwa kingono na mama yake mzazi ili kupata fedha za kukidhi mahitaji ya familia. Endelea kufuatilia kupata undani wa mustakabali wake.**

--------------------------------

**HATUA SERIKALINI**

KINACHOSHUHUDIWA na gazeti hili wilayani Kinondoni, ni sura nyingine ya ukatili wa jinsia na madhila yanayowakabili watoto, Ofisa Ustawi wa Jamii Kata ya Mwananyamala, Edith Mligo akikiri kuwa na taarifa za yanayotendeka dhidi ya kundi hilo kwenye eneo lake la kazi.

"Kesi za aina hii zipo, huwa tunazisikia lakini ushahidi wake ni mgumu kwa sababu wengi wao wanafanya biashara hiyo kwa siri na sisi tunategemea zaidi kupata yaliyojificha kutoka kwa wazazi.

"Shida inakuja pale mzazi anapofaidika na hilo, hawezi kuleta taarifa ofisini kwetu. Tunatambua mambo hayo yapo na yanafanyika kwa siri

"Hii ni tabia hatarishi kwa sababu mtoto aliyefanya hivyo, akapata fedha, akanunua simu, watoto wengine wanaweza kushawishika na kuiga. Kwa hiyo, itachangia watoto wengi kujiingiza humo na hivyo kupoteza nguvukazi ya taifa.

"Huo ni ukatili kwa sababu mzazi anadhani anapata manufaa lakini anamuumiza mtoto, anafanyishwa kitu ambacho kinamwathiri ubongo wake kwa sababu kwa umri huo alitakiwa awe shuleni.

"Ustawi wa Jamii tutakapoletewa kesi kama hiyo na wasamaria wema, lazima huyo mzazi achukuliwe hatua za kisheria, kwa sababu huo ni ukatili, huko mtoto anakutana na mambo mengi yanayokiuka haki ya mtoto. Kesi kama hii ikija lazima niisimamie kidete kwa sababu huo ni zaidi ya ukatili," anasema.

Judith anayekemea utumikishwaji huo wa watoto, anatoa raia kwa wakazi wa Mwananyamala kuwafichua wazazi wote waliopotoka kimalezi na kuamua kuwatuma watoto wao kufanya vitendo hivyo.

"Serikali inapingana na hilo, hata dini zetu hazijabariki hilo, kumuuza mtoto ni kosa kisheria. Kwa kutambua hilo, wanafanya vitendo hivyo kwa kificho wakijua sheria itachukua mkondo wake," anasema.

Judith anasema mbali na kadhia hiyo, Mwananyamala pia ina matukio ya ubakaji na ukatili wa kijinsia, akibainisha kuwa katika miezi 10 ya mwanzo ya mwaka huu, yaani Januari hadi Oktoba, visa saba viliripotiwa ofisini kwake na tayari kuna kesi zinaendelea kwenye vyombo vingine vya kisheria.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Watoto, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Dar es Salaam, Nyamala Elisha anasema kuwapo kesi za aina hiyo si ngeni ofisini kwake japo hana taarifa zilizoripotiwa ofisini kwake kuhusu binti wa Mwananyamala anayetumiwa na mama yake mzazi.

"Kwa mazingira ya sasa hatuwezi kuliona hilo kama suala geni katika jamii ambayo baba anamnajisi mtoto wake wa kumzaa, mjomba anambaka mtoto wa dada yake, dunia imebadilika.

"Lakini kwanini hao wanajamii wanayaona hayo yakitendeka na wanakaa kimya? Hapo ndipo tunarudi kwenye Sheria ya Mtoto kifungu cha 95 kinachoeleza mwanajamii yeyote atakayeshuhudia hilo na akakaa kimya, itakapobainika atachukuliwa hatua.

"Kwa hiyo, ninafikiri hapo tunapaswa kunyoosha kidole kwa wazazi, walezi na jamii kwa sababu mambo hayo yanafanyika hadharani na watu wanayaona.

"Hatuwezi kuwa na ofisa ustawi wa jamii kila nyumba au kila mtaa, ulinzi mkubwa wa nchi kwenye jambo lolote lile upo kwa wanajamii wenyewe.

"Sasa kama jambo linafanywa na wazazi kwa kificho, usiri unakuwa mkubwa, ni vigumu kulifahamu hili mpaka mwanajamii atakapojitokeza kutuletea taarifa.

"Ustwai wa jamii tunafanya kazi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi. Sisi tunashughulika zaidi na mtendwa, wao (polisi) wanashughulika na mtenda.

"Utaratibu ni kwamba kile ni kitendo cha kihalifu, hivyo katika hilo ofisa ustawi huwezi kwenda pale kama anashughulikia uhalifu, ni lazima aongozane na polisi.

"Hata ukirudi katika Sheria ya Mtoto kifungu cha 94(3), inaelekezwa kwamba itakapothibitika, ofisa ustawi wa jamii akiwa ameambatana na Jeshi la Polisi watakwenda kuona mazingira. Na kama ni kweli, sisi tutaoa elimu huku polisi wakiendelea na hatua zao za kipolisi za kijinai," anafafanua.

Anataja hatua wanazochukua kukabiliana na vitendo hivyo, zinajumuisha kutoa elimu kwa wazazi na waathirika wa vitendo hivyo ili watambue madhara yake na kuhamasisha jamii kupaza sauti kukemea vitendo hivyo na kutoa taarifa za matukio ya kikatili.

"Wazee, wachungaji, mashekhe, wasanii na waandishi wa habari tuungane kwa pamoja, kila taasisi kwa nafasi yake, kukemea vitendo hivi ili kukinusuru kizazi kilichopo na kijacho," anashauri.

Alipotafutwa na Nipashe juzi kuzungumzia kadhia hiyo, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro alisema:

"Hizi taarifa ndiyo kwanza ninazisikia kutoka kwako (mwandishi wa Nipashe), tutafuatilia".




Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam Jumanne Muliro

**WADAU & SHERIA**

Mkurugenzi wa Taasisi ya Wajiki inayojihusisha na utetezi wa haki za wanawake na watoto yenye makazi yake Mwananyamala, Janeth Mawinza, ana ushuhuda wa matukio ya aina hiyo kwenye eneo lake la uwajibikaji, akiitaka jamii kukemea na kuwafichua wanaoendekeza madhila hayo dhidi ya watoto ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

"Sisi tunashughulika na kupiga vita masuala ya rushwa ya ngono lakini pia huwa tunajihusisha na kulinda haki za watoto. Katika kazi zetu hizi tuliwahi kukutana na kisa kama hicho lakini huyo mtoto alikuwa anaishi na dada yake.

"Baada ya kuletewa kesi hiyo, tulifuatilia na kubaini ukweli wake, tukamchukua mtoto, tukamsafirisha kurudi kwao Mbeya kwa wazazi wake. Mambo haya hapa Mwananyamala yapo," anasema.

Wakili wa Kujitegemea kutoka Kampuni ya Accuracy yenye maskani yake Kinondoni, Bashiru Yakubu, anatoa tafsiri ya kisheria kwamba ni kosa mzazi kumtumikisha mtoto kingono.

"Hili ni kosa la ukatili wa kingono kwa mtoto na adhabu yake inaweza kuwa kifungo cha miaka mitano hadi saba gerezani.

"Kwa yule mtu anayemnunua mtoto huyo atashtakiwa kwa kosa la ubakaji kwa sababu kwa mujibu wa sheria, ukifanya mapenzi na mwanamke ambaye hajafikisha miaka 18 (mtoto), hata kama mmekubaliana, unatafsiriwa kama mbakaji na adhabu yake inaweza kuwa hadi kifungo cha miaka 30 jela.

"Kama huyo mbakaji katika kutenda kosa hilo atakuwa amemwingilia kinyume cha maumbile, ikithibitika adhabu yake ni kifungo cha maisha gerezani," anafafanua Wakili Yakubu.

Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, pamoja na mambo mengine, inaelekeza wajibu wa serikali, wazazi, walezi na jamii kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vyote vya ukatili na ubaguzi.

## HABARI KITAIFA

# Bilioni 270/- kutumika mradi wa shule bora

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI ya Uingereza kupitia mfuko wa UK Aid imepanga kutumia Sh. bilioni 271 kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Shule Bora ambao utatekelezwa katika mikoa tisa nchini ili kuinua viwango cha elimu katika mikoa hiyo.

Mkuu wa Kitengo cha Huduma ya Jamii Ubalozi wa Uingereza, Getrude Mapunda, akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa ofisi ya mradi huo mkoani Singida, alisema utatekelezwa hadi ifikapo mwaka 2027.

Alisema mradi huo umelenga kuiunga mkono Serikali ya Tanzania katika kuinua kiwango cha elimu jumuishi pamoja na kuweka mazingira salama ya kujifunzia kwa wanafunzi wa kike na kiume katika shule za serikali zilizopo katika mikoa hiyo.

Mapunda aliitaja mikoa ambayo Mradi wa Shule Bora utatekelezwa ni Singida, Dodoma, Simiyu, Tanga, Mara, Rukwa, Katavi, Pwani na Kigoma, ukilenga kuboresha maeneo ya kujifunzia, kufundishia, jumuishi na kujenga mfumo.

"Mradi wa Shule Bora utafanya maboresho yatakayowezesha kila mtoto kupata msingi mzuri katika elimu yake ili kuitumia fursa kwa kutoa mchango wake katika ukuaji wa nchi na maendeleo yake," alisema.

Mapunda aliongeza kuwa mradi hauanzishi vitu vipya, bali unatekeleza mipango ya halmashauri ili kuunganisha rasilimali fedha na rasilimali watu kutoka serikali na mwenye mradi ili kuwasaidia watoto wa kitanzania.

"Mradi hauna fedha nyingi kuliko za serikali, hivyo tukichanganya fedha nyingi za serikali na zile kidogo za mradi tunaweza kufikia malengo ya halmashauri zilizojiwekea katika kuboresha elimu ya msingi na sekondari," alisema.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Stanslaus Choaji alisema uzinduzi wa ofisi ya mradi huo mkoani hapa ni juhudi za serikali kwa kushirikiana na wadau hao kuboresha ujifunzaji, ufundishaji na ujumuishi wa elimu ya msingi na sekondari.

Choaji alipongeza timu ya Mradi wa Shule Bora kwa namna ambavyo imeanza kutekeleza majukumu yake mbalimbali kupitia halmashauri za mkoa huo.

Aliahidi kwa niaba ya Mkoa wa Singida kushirikiana na wadau hao kufanikisha mipango waliojiwekea ili kumkomboa mwanafunzi ndani ya Singida na Taifa kwa ujumla.

Mratibu wa Mradi wa Shule Bora Mkoani Singida, Samweli Daniel alisema kuwapo ofisi hizo kutasidia katika utekelezaji wa majukumu yao na watahakikisha vikwazo vinavyokabili elimu mkoani hapa vinakwisha na watoto wanapata elimu bora kwa usawa.



Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Ally Kijazi, akipanda mti wa kutunza mazingira katika kijiji cha Potwe, wilayani humo juzi, katika kilele cha maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Wengine waliosimama ni Mhifadhi Mkuu Msaidizi wa Misitu wa wilaya hiyo, Jackson Saria (kulia), Diwani wa kata ya Potwe, Othman Bahari (wa pili kulia), Ofisa Tawala wa wilaya, Hadija Nassoro na Ofisa Mazingira wilaya, Cyprian Mselem. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# REA kuwezesha mfumo gesi asilia mikoa miwili

**Na Ashton Balaigwa,** KILOMBERO

WAKALA wa Nishati Vijijini (REA) umesema kuwa mwakani unatarajia kusambaza mifumo ya mabomba ya gesi asilia majumbani kwa wananchi wa mikoa ya Pwani na Lindi ili kuongeza kasi ya kuondokana na uharibifu wa mazingira unaotokana na matumizi ya kuni na mkaa.

Mkurugenzi Mkuu wa REA, Hassan Saidy aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa miradi ya kusambaza nishati vijijini iliyofanyika katika Mradi wa Kituo cha Kupoza na Kusambaza Umeme cha Ifakara wilayani Kilombero mkoani Morogoro.

Alisema mradi huo wa majaribio utahusisha vijiji vya mikoa hiyo na utafanywa kwa ushirikiano kati ya REA na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

Saidy alisema katika kuunga mkono jitihada za matumizi ya nishati jadidifu, wanafadhili TPDC zaidi ya Sh. bilioni sita ili kusambaza mfumo wa gesi majumbani katika vijiji vya mikoa hiyo.

Alisema wamesaidia mradi huo kutokana na utafiti uliofanywa kuonyesha zaidi ya asilimia 80 ya matumizi ya nishati hutumika kupikia wakati iliyobaki hutumika kwenye matumizi mengine ikiwamo viwanda. Alisema kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB), wamelenga kusambaza majiko banifu 200,000 na kuwajengea mitambo ya kuzalisha baiyogesi katika taasisi za umma zinazohudumia kuanzia watu 300 ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Alisema utafiti unaonyesha ukipikia kuni na mkaa kwa siku ni sawa na kuvuta sigara 300.

Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Habari Maelezo, Rodney Thadeus alisema mradi wa REA katika ukanda wa Morogoro utasaidia kuhamasisha kilimo mkoani hapa na maeneo mengine ya jirani.

# UWT kumsaidia Rais Samia kuwajibika viongozi wazembe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Mary Chatanda amesema hatasita kuwashughulikia wanawake viongozi, wakiwamo mawaziri, watakaothibitika kuonyesha uzembe na kutokuwa waadilifu kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

Akizungumza juzi jijini kwenye kongamano la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa kwa mwaka 2022 hadi 2027, Chatanda alisema: "Hatutasita kukemea maovu wanawake wenzetu viongozi ambao wataonyesha uzembe na kutokuwa waadilifu wakati wa kutekeleza majukumu yao.

"Na ikibidi tutapendekeza hatua za kuchukuliwa endapo tutaona na kuthibitisha vitendo vyovyote vinavyoashiria uzembe, kukosa maadili, hujuma kwa kiongozi yeyote mwanamke dhidi ya serikali kwenye hii ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia."

Alisema wanataka wanawake wote nchini kuonyesha kiwango cha juu cha uwajibikaji kwa nafasi walizonazo ndani ya chama na serikali kuliko wakati mwingine wowote. Alisema UWT inakwenda kuhakikisha jumuiya hiyo inaanzisha miradi na kutekeleza iliyopo ili kujitegemea na mambo yote yaliyoelekezwa na Mwenyekiti Samia.

"Katika kipindi miaka miwili ya uongozi wa awamu ya sita, tuna nguvu ya kusimama na uongozi wa juu wa nchi kama wanawake walivyokuwa mbele kudai uhuru wa nchi. Kwa wanawake wa sasa ambao tunafaidi matunda ya uhuru waliopigania waasisi wetu, hatuna budi kuendelea kuonyesha uthubutu, kuwa mstari wa mbele na kumuunga mkono Rais katika jitihada za kuiletea maendeleo nchi," alisema.

Alisema watahakikisha wanaunga mkono serikali na kuzisemea kazi za serikali kwa pande zote mbili za Muungano.

"Sisi kama UWT ambao ndiyo wengi nchini kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi, tunapaswa kutumia fursa ya utekelezaji mzuri wa ilani kwa maendeleo ya ustawi wa wanawake.

"UWT tunakwenda kuhamasisha uthubutu wa wanawake katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, kisiasa na kijamii na kuhamasisha wanawake katika nafasi za uongozi kuwajibika kwa nafasi mbalimbali kwa weledi, uadilifu na uchapakazi ili kumsaidia Samia kuanzia ndani ya jumuiya, chama na serikali," alisema.

Spika mstaafu wa Bunge la Afrika, Getrude Mongela, alisema enzi zao mtu akiteuliwa kuwa waziri, alikuwa anasali na endapo mtu akikosea anageukwa na wanawake na taifa zima wakisema 'unaona wanawake'.

"Tutamsaidie Rais Samia azibe mwanya wa wanawake, tunataka waseme 'wanawake mnawaona kwa ufanisi na utekelezaji?', tusimwachie peke yake ataelemewa na mtaanza kumgeuka hata nyie na kusema ametufungia milango, hii nafasi tuitendee haki, ni yetu wanawake, tunataka waone na waseme 'tumechelewa kuwaweka wanawake'," alihimiza. Alishauri uongozi wa UWT Taifa kuweka mikakati ya kuwajenga vijana wanawake ili waipende jumuiya hiyo.

"Nilipofika hapa nimetishwa na nguvu ya wanawake, nikajiuliza hivi nani atatuzuia kushika hatamu. Wanawake wanatakiwa kutokuwa na uoga wa kuisemea nchi, mama Chatanda uende usiogopa, umpe majina sio kusubiri wanaume ndio wapeleke, nenda kwa heshima na adabu na useme kazi zilizofanyika," alisema.

Awali Mwakilishi wa Mawaziri Wanawake na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki alisema ushindi alioupata Rais Samia unatokana na maboresho makubwa aliyofanya ndani ya chama na jumuiya zake na mafanikio makubwa, uongozi mahiri, uadilifu, uchapakazi na kusimamia kile anachokiamini. Akisoma maazimio ya UWT ya kumpongeza Rais Samia, Mbunge wa Viti Maalum, Neema Lugangira alisema wanampongeza kwa kufanya kazi nzuri ambayo wanawake watamsemea, kumpigania na kumpambania.

"Tutakuwa mstari wa mbele kuwatafuta, kuwashawishi, kuwalea na kuwajengea uwezo mabinti na wanawake kugombea na kuwainua katika nafasi za uongozi na tutapinga aina zote za ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto nchini," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Matumizi bidhaa za ndani iwe agenda ustawi viwanda

**SHIRIKISHO** la Wenye Viwanda Tanzania (CTI) wiki hii lilifanya mkutano wake wa mwaka ambao pamoja na mambo mengine, lilisisitiza umuhimu wa uzalishaji wa bidhaa za ndani zenye ubora kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya viwanda.

Katika msisitizo huo, liliweka bayana kwamba Watanzania wanapaswa kuzalisha bidhaa zenye ubora ili kuviwezesha viwanda kuzitumia kwa ajili ya utengenezaji wa bidhaa mbalimbali badala ya kuendelea kuagiza bidhaa kama hizo kutoka nje ya nchi.

Mwenyekiti wa CTI, Paul Makanza, katika ufunguzi wa mkutano huo, alisema Tanzania ina malighafi nyingi ambazo zinaweza kutumika kutengeneza bidhaa za aina mbalimbali na zenye ubora wa hali ya juu na kwamba hali hiyo itasaidia kuondokana na utegemezi wa kuagiza bidhaa nyingi nje ya nchi hali ambayo inaweza kudhoofisha viwanda vya ndani.

Pamoja na shirikisho hilo kusisitiza matumizi ya malighafi za ndani, hata wakati wa maonyesho ya bidhaa za ndani yaliyomalizika juzi katika Viwanja vya Maonyesho ya Biashara vya mwalimu Nyerere, Dar es Salaam, hamasa kubwa ilikuwa matumizi ya bidhaa zinazotengenezwa nchini ili kuinua uchumi wa taifa.

Hatua hiyo ya CTI kusisitiza matumizi ya malighafi za ndani ni ya msingi kwa ajili ya maendeleo ya viwanda na uchumi kwa ujumla. Ni hakika kwamba matumizi ya bidhaa au malighafi hizi, yatasaidia katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa hali na wa kipato.

Ni dhahiri kwamba malighafi za ndani zinapotumika katika uzalishaji viwandani, mnyororo wa thamani kutoka kwa mkulima mpaka kwa mtumiaji unaimarika sambamba na kupunguza umaskini walio nao wananchi na wakati huo huo ajira mbalimbali zitaongezeka na kutatua tatizo hilo ambalo linawakabili wananchi hasa vijana.


Kwa muda mrefu, wakulima wa mazao ya biashara na chakula wamekuwa wakilalamika kwamba hawana masoko kwa ajili ya bidhaa na malighafi zao. Hatua ya CTI kusisitiza hilo, kilio cha wakulima hao kitapungua hata kumalizika kabisa kwa sababu hawatakuwa na sababu ya kuendelea kulia ilhali soko la uhakika lipo. Kwa mantiki hiyo, wakulima na wazalishaji wa bidhaa ambazo husaidia kuzalisha bidhaa zingine viwandani wanatakiwa kuchangamkia fursa hiyo kwa kujikita katika uzalishaji ambao utatosheleza kwa kiasi kikubwa mahitaji ya malighafi katika viwanda vya hapa nchini.

Licha ya CTI kusisitiza hilo, ni jambo la aibu kwa Tanzania ambayo ina ardhi ya kutosha wamiliki wa viwanda kuagiza malighafi na bidhaa za kulisha viwanda vyao kutoka nje. Jambo la kujiuliza, kwa mfano, kwa ardhi iliyo nayo ina ulazima wa kuagiza malighafi kutoka nje kwa ajili ya viwanda vya kuzalisha mafuta ya kula?

Suala la uagizaji wa bidhaa na malighafi kutoka nje lilianza wakati wa ubinafsishaji miaka ya 1990 hali iliyosababisha bidhaa za ndani kuporomoka na kukosa soko kwa madai kwamba hazina ubora.

Mfano mmoja ni wakati wa ubinafsishaji wa viwanda vya vinywaji hasa bia. Baada ya mchakato huo kukamilika, wawekezaji hao walitamka kuwa ngano iliyokuwa ikizalishwa nchini ilikuwa chini ya kiwango na pia chupa zilizokuwa zikitumika kuweka vinywaji hivyo zilikuwa hazina ubora, hivyo kulazimika kuagizwa kwa bidhaa na malighafi hizo kutoka nje.

Matokeo ya kufanyika hivyo ni kwamba mashamba makubwa ya ngano Mbulu na Hanang mkoani Manyara yalifungwa na viwanda vya chupa vilikosa soko. Kama ilivyosisitiza CTI, suala la matumizi ya malighafi za ndani kwa ajili ya viwanda vyetu linapaswa kuwa ajenda endelevu.






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wabongo tutunze afya kwa mazoezi

Na Adam Fungamwango

**KUMEKUWA** na kasi ya ajabu nchini ya magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo kisukari na shinikizo la damu kwa wananchi wa kawaida tu, ambapo kwenye miaka ya nyuma yalichukuliwa kama ni magonjwa ya matajiri.

Miaka ya 1990 kurudi nyuma ilikuwa si rahisi kumuona mwananchi wa kawaida anakwenda hospitali anaumwa magonjwa hayo. Yalikuwa ni ya watu wenye hadhi fulani hivi, matajiri na wengine wanaofanana na hao.

Kila miaka inavyozidi kusonga mbele hali inabadilika. Kwa sasa umekuwa ni ugonjwa unaowapata hata watu wa kawaida na wenye kipato cha kawaida pia. Tatizo ni nini?

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Prof. Abel Makubi anasema hii inatokana na mtindo wa maisha, kutofanya mazoezi pamoja na matumizi ya pombe na sigara kupita kiasi.

Anasema mbali na mazoezi, lakini pia ulaji wa vyakula vingi vya mafuta pia vinasababisha ongezeko la wagonjwa wengi wa maradhi yasiombukizwa.

Akasema takwimu za wagonjwa wa maradhi yasiyoambukiza nchini zimekuwa zikipanda kila mwaka hali ambayo inatishia nguvu kazi ya taifa.

Profesa huyo aliongea maneno hayo juzi jijini Dodoma akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumaliza kufanya mazoezi yaliyoandaliwa na wizara hiyo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

"Mwaka 2017 takwimu za wagonjwa walioripoti katika hospitali zetu ilikuwa takribani milioni 2.5 lakini hadi mwaka 2021 imeongezeka hadi milioni 3.5 sawa na ongezeko la asilimia tisa.

Hawa ni wale tu walioripoti katika hospitali na vituo vya afya. Lakini wapo wengine ambao labda walikwenda kwa waganga na wengine wako majumbani, hivyo hali inaonekana bado ni tishio kwa taifa," anasema.

"Kutokana na hali hii wananchi wanapaswa kubadili mtindo wao wa maisha kwa kuanza kufanya mazoezi angalau kwa siku nne za wiki ili kujikinga na magonjwa haya yasiyo ya kuambukiza," anasema.

Sasa hapa unajiuliza kwa nini zamani watu walikuwa wanavuta sigara na kunywa pombe kama hawa wa sasa, lakini walikuwa hawapati sana magonjwa haya?

Tunarudi pale pale, ni mtindo wa maisha. Zamani watu walikuwa wanatembea umbali mrefu kwa miguu. Hakukuwa na barabara bora, usafiri wa uhakika, bajaj wala bodaboda. Pia hakuweza kumiliki magari binafsi. Hii iliwasaidia sana kutembea umbali mrefu kwa hiyo hata kama amekula chakula kingi chenye mafuta kinayeyuka na kufanya kazi haraka.

Na hili linaonekama hata leo, wanaoishi vijijini wanakuwa na afya njema kuliko wa mijini. Na ndiyo wanaoishi maisha marefu kutokana na kazi nyingi wanazofanya kuwa kama mazoezi kwao.

Hata hivyo sigara na pombe nazo zinachangia kwa kiasi kikubwa maradhi hayo.

Pia kula sana. Kuna watu wanapenda kula sana vyakula vyenye mafuta na vyenye gharama kubwa wakidhani kuwa ni dalili ya kuonekana ana uwezo wa kifedha kumbe anajimaliza.

Kwa sasa tuna kizazi chenye kila dalili ya uvivu. Hakipendi kutembea kwa umbali mrefu. Kibaya zaidi hupenda kula chakula ambacho kitawavutia wengine kukitazama na kuonekana ana pesa, na si kile ambacho kinakwenda kufanya kazi ya kumletea afya mwilini.

Nilichogundua ni kwamba vyakula vingi bora na vya kuzuia uwezekano wa kuwa na magonjwa mwilini vingi havina gharama kubwa na havina ladha nzuri mdomoni.

Kama alivyosema mtaalam wa masuala ya afya ni kwamba Wabongo tubadilike. Tuwe na utaratibu wa kufanya mazoezi, kupunguza matumizi ya sigara na pombe, kula vyakula ambavyo vitatuletea afya mwilini, si vitamu mdomoni.

Vinginevyo namba za wagonjwa wa magonjwa yasioambukizwa itaongezeka, nchi itakuwa na wagonjwa wenye miaka 30 tu. Nchi itaanza kupoteza raslimali watu, kwani watu wanaweza kupoteza maisha wakiwa na umri mdogo tu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## SAFU

### KWA MASLAHI YA TAIFA

# Miaka 61 ya uhuru tumefanikiwa na tumekwama wapi?



Pascal Mayalla

DESEMBA 9, Watanzania tuliadhimisha miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika (sasa Tanzania Bara). Kiukweli tumefanikiwa sana katika mambo mengi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii lakini pia lazima tukubali kwamba hapa tulipo, sipo mahali tungepaswa tuwe. Tulipaswa kuwa mbali zaidi ya hapa tulipo, hivyo 'Kwa Maslahi ya Taifa', inatafakari kwa juu juu, tulipaswa kuwa wapi na tunakwama wapi?

Tulipopata uhuru mwaka 1961, tulikuwa tunakabiliwa na maadui wakuu watatu wa taifa, ambao ni ujinga, umasikini na maradhi, hivyo tukatangaza vita dhidi yao. Leo miaka 61 ya uhuru, si tu maadui hao wangalipo, bali tumeongeza maadui wengine wawili ambao ni rushwa na ufisadi. Maadui hawa wawili hawakuwapo wakati tunapata uhuru.

Kwa adui ujinga, wakati tunapata uhuru, nchi ilikuwa na majimbo, elimu ilikuwa ya kulipia. Watoto wa kutoka majimbo yenye mazao ya biashara, yakiongozwa na kahawa, hivyo watu wa Kagera, Kilimajaro, Arusha na Mbeya, ndio watoto wao walisoma kwa sababu wazazi wao waliweza kulipa karo ya shule. Jimbo la Nyanza, lenye mikoa ya Kanda ya Ziwa, wao walikuwa na Pamba, Tanga wakasomeshwa na Katani. Mikoa isiyokuwa na mazao ya biashara kama Singida, Dodoma, mikoa ya kusini na Pwani, wao waliokolewa na kusomeshwa na wamisionari katika shule za seminari.

Hivyo makabila kama Wahaya, Wachaga na Wanyakyusa wengi walipata fursa za kujiendeleza kielimu na kuonekana kama makabila haya wana akili sana kutokana na uwezo wa kulipiwa karo.

Rais wa Tanganyika, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kwa kulijua hili, akatangaza elimu bure, kuanzia darasa la kwanza hadi chuo kikuu. Hii ikafungua fursa za elimu kwa wote na tuliendelea kufanya mitihani inayotungwa Cambridge, Uingereza. Hata baada ya kuanza elimu bure, bado waliopasi wengi mitihani hiyo, walikuwa watoto wa makabila yale yale.

Tukaachana na mitihani ya wazungu, tukaanzisha baraza letu la mitihani, tukatunga wenyewe mitihani rafiki. Lakini bado waliopasi wengi ni kutoka makabila yale yale!. Ili watu wa makabila yote wapate fursa sawa za kujiendeleza, serikali ya Nyerere ikaamua kuweka viwango tofauti tofauti vya ufaulu kwa baadhi ya mikoa na kwa mikoa mingine viwango vikashushwa mpaka chini ya alama 50 ili kila Mtanzania aingie sekondari. Hii ikasaidia watoto wa makabila yote kuingia sekondari.

Kwa yale makabila ya hali ya chini sana kama Wahadzabe na Wataturu, hawa hawakujua shule, hawaongei lugha ya Kiswahili na wanaishi maporini, serikali iliwakamata kwa nguvu watoto wa familia hizo, na kuwapeleka kwa nguvu shule za bweni na kusomeshwa chini ya ulinzi.

Japo wote hawakufaulu hata kiwango cha chini kabisa, bado serikali iliwaingiza sekondari kwa nguvu kwenye shule za bweni. Mwanzo ilianza na Ilboru, wenzao wakawa wanawaona na kuwatorosha wote, ndipo serikali ikawapeleka Shule ya Sekondari ya Pugu. Hapo walisoma mpaka kidato cha nne, japo wote hawakufaulu, angalau walijua kusoma, kuandika na ustaarabu wa kuvaa nguo.

Serikali ikawarudisha kujiunga na jamaa zao kwa kuwapa na zawadi za nguo nyingi za kuwavisha jamii nzima, wakawaacha kijijini kwao. Baada ya mwezi, wakaenda kuwatembelea kukagua maendeleo yao, walishangaa si tu zile nguo walizikuta pale pale walipowaacha, bali hata nguo za wale waliosomeshwa na kustaarabika nao walizivua na kuziacha pale pale na kuvaa mavazi yao ya asili!

Juhudi za serikali ya awamu ya kwanza kupambana na adui ujinga ziliendelea kwa kuanzisha elimu ya watu wazima, kisomo cha ngumbaru na kuibadili mitaala ya elimu kuwa na elimu ya kujitegemea na kuanzisha vyuo vya ufundi nchi nzima. Elimu ya mkoloni ililenga kupata makarani lakini baada ya uhuru tukaanzisha elimu ni kazi, elimu ya kujitegemea, ili lengo la kuelimika si tu ili kuajiriwa bali kujiajiri.

Kuna kipindi, Tanzania ilikuwa nchi kiongozi barani Afrika kwa 'literacy level' ya watu wanaojua kusoma na kuandika. Hiki kiwango kwa sasa kimeshuka, sijui tunakwama wapi? Kwa sasa karibu kila kata ina shule ya sekondari, kila mkoa kuna vyuo vya ufundi stadi.

Tulipopata uhuru, tulikuwa na chuo kikuu kimoja tuu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa jina maarufu UDSM na fani ya kwanza ilikuwa sheria. Sasa tuna vyuo vikuu vingi na fani nyingi, tunatoa wahitimu wengi na tuna maprofesa na madaktari wa falsafa (Ph.D) wa kutosha kutoka vyuo vikuu vya kuheshimika na kueleweka hadi vyuo vikuu vya mtandaoni, ambavyo vinatoa Ph.D hata kwa darasa la saba!

Majuzi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kimemtunuku Rais Samia, shahada ya heshima ya udaktari wa falsafa, iitwayo Honoria Causa, hivyo Rais Samia sasa anatambulika kama Daktari Samia Suluhu Hassan. Kwa kuwa sasa anatambulika kama daktari, nashauri lile jina la Mama Samia, sasa life, libaki ofisini kwake, nyumbani kwenye familia yake na kwa watu wake wa karibu. Nami niungane na Watanzania wenzagu kumpongeza Rais Samia kutunukiwa shahada ya heshima ya udaktari wa falsafa kutokana na kazi nzuri anayoifanya kwa maslahi ya Watanzania. Ni heshima kubwa kwako na kwa taifa kwa ujumla.

Ni kweli Rais Samia amepewa udaktari wa heshima kutokana na sifa kedekede zilizoainishwa wakati akitunukiwa ambazo wale wanaofuatilia masuala ya nchi yetu watakubaliana na waliompatia. Lakini swali langu bado liko kwa maprofesa na madaktari waliojaa kila kona nchini, je, wanalisaidiaje taifa letu kusonga mbele? Tunakwama wapi?

Naomba kwa leo niishie hapa. Wiki ijayo nitaangazia miaka 61 ya uhuru kwenye mapambano dhidi ya adui umaskini. Kiukweli Watanzania wengi bado ni maskini. Je, tunakwama wapi?

**Nawatakia heri ya Uhuru na Jamhuri. Paskali 0754 270403**

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Mishahara kupanda ni jambo moja, utekelezaji ni lingine



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

HATIMAYE serikali imetangaza kima kipya cha mishahara ya chini kwa sekta binafsi nchini na kikitarajiwa kuanza kutumika Januari, mwakani. Mara ya mwisho kutangazwa kwa kima hicho ikiwa ni 2013.

Tangazo hilo bila shaka limepokewa kwa furaha na waajiriwa huku likipokewa kwa majonzi na baadhi ya waajiri ambao kwao daima ni kunyonya na kukandamiza wafanyakazi wao.

Ongezeko hilo la mishahara kima cha chini, linatoka huku nchini fursa za ajira zikiwa finyu kwani vijana wengi wako mitaani wakizurura kutafuta ajira isiyopatikana.

Badala yake wamekuwa wakitiwa moyo na viongozi wa kujiajiri, ikidhaniwa pengine mitaji iko bwerere na baadhi yao wakisisitizwa kusubiri na kuomba mikopo ya halmashauri ambayo nayo hutoka kwa kutazamana nyuso na sura.

Sekta 12 zimeguswa na mabadiliko hayo ya mishahara yaliyotangazwa na Waziri mwenye dhamana ya Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Profesa Joyce Ndalichako. Sekta hizo ni za kilimo, afya, mawasiliano, kazi za majumbani, hotelini na ulinzi binafsi.

Zingine ni nishati, usafirishaji, ujenzi, madini, shule binafsi, biashara na viwanda, uvuvi na shughuli za baharini na mwajiri ruksa kumlipa mfanyakazi wake zaidi ya kima kilichotangazwa na kamwe si chini yake.

Waajiriwa wote watafurahia kwani ni neema angalau kutoka kiwango fulani kupanda hadi kingine. Lakini kama nilivyosema hapo awali, waajiri lazima watanuna kwani wengi hawapendi kuona wanapungukiwa.

Hawaamini katika Mungu atarejesha ulikopunguza na kuongezewa, wao wanaamini kingine kisitoke. Ndiyo maana kutatokea jambo katika baadhi ya sekta.

Mathalan wafanyakazi wa baa na majumbani kwa kweli ndio huonewa sana na waajiri wao, kwa sababu za kikatili tu kana kwamba ni watu wasio na manufaa katika jamii na hivyo kujikuta wakilipwa kidogo.

Hata serikali katika hili, imesema mfanyakazi wa ndani anayeishi na mwajiri wake atalipwa Sh 60,000 ila anayetoka kwao atalipwa Sh 120,000! Fikiria Sh 60,000 kwa mwezi eti kwa sababu tu anakula kwa mwajiri! Wale wa baa, watalipwa si chini ya Sh 150,000. Kwa wasiojua, kada hii ni muhimu sana katika maisha na ustawi wa jamii!

Nakumbuka katika utawala wa Rais John Magufuli, ulitangazwa muda wa kufunguliwa kwa baa nchini kwamba uwe saa 10 jioni na kufungwa saa sita usiku. Kilichotokea kila mtu aliona jinsi waajiri walivyopunguza wafanyakazi.

Walikuwa na haki ya kufanya hivyo kwa sababu wateja walipungua, hivyo kushindwa kulipia kodi, maji, umeme na mishahara ya wafanyakazi na mambo mengine madogo madogo, ikiwamo gesi kwa ajili ya jikoni.

Leo kwa kuwa mishahara imeongezwa, ina maana kwa athari za amri ya Magufuli, bado baa nyingi hazijasimama vyema. Wateja wamepungua, hivyo kiingiacho nacho kimepungua. Je, waajiri hawatapunguza nguvukazi ili kubaki na kipato kile kile au kuongezeka kidogo?

Imekuwa kawaida serikali kutangaza viwango vya mishahara kwa sekta hizo, bila kufuatilia utekelezaji wake, hivyo kuacha waajiriwa wakinung'unika chinichini, wasijue la kufanya au hata wakikosa pa kwenda.

Hayo yanatokea pia kwa wafanyakazi wa ndani na hasa walao kwa waajiri wao ni hali ngumu wakikabiliwa na manyanyaso na wakionekana wao na wenzao wa baa kama watu wasio na pa kwenda. Na hilo limekuwa likitumiwa sana na waajiri. "Mtapata wapi ajira?"

Hivyo serikali isiishie kutangaza kima cha chini na kusema mwajiri asilipe chini ya hapo, huku ikiacha kufuatilia utekelezaji na hivyo nyongeza kuonekana silaha ya kuumiza waajiriwa hao. Profesa Ndalichako hapa sasa ndipo pa kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan yeye na serikali yake wasichukiwe na wananchi.

Kama hili, pia afuatilie na taasisi, kampuni na mashirika na hata waajiri binafsi wasiopeleka michango ya waajiriwa wao kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, wakiwamo wahudumu wa baa na wafanyakazi wa ndani majumbani. Bila kufanya hivyo haitakuwa na maana ya kuwa na wizara yenye dhamana.

**Alamsiki!**

## Ashauri usomaji wa vitabu kuepuka msongo mawazo

**Na Halfani Chusi**

OFISA Mtendaji Mkuu Ofisi ya Hakimiliki Tanzania, Doreen Sinare amewataka wanafunzi kujenga utamaduni wa kusoma vitabu ili kujiongezea maarifa na kupunguza msongo wa mawazo.

Alitoa rai hiyo mkoani Dar es Salaam jana alipozindua kitabu kilichopewa jina la 'Kadogoo Mtalii' kilichotungwa na mchoraji katuni maarufu za kadogoo, Francis Bonda 'Kaka Bonda'.

Uzinduzi huo ulihudhuriwa na wanafunzi wa shule za awali na msingi walioimba na kucheza eneo la Mikocheni wilayani Kinondoni.

Doreen alisema kitabu hicho kimeelezea hadithi za mambo yanayohusu Tanzania, akiwahimiza wazazi na shule mbalimbali kuwanunulia wanafunzi wao ili wafahamu maudhui yaliyowasilishwa.

"Nilichofurahi zaidi ni kuona watoto wametoka sehemu tofauti tofauti, kuna wengine wametoka katika vituo vya ubunifu, yaani watoto ambao wana vipaji maalum, nimeona wanaimba hapa mpaka mwili unasisimuka.

"Kwa hiyo, sisi kama taasisi tuna kila haja ya kuwainua katika mradi wetu, tupo katika hatua za mwisho baada ya hapo tutatembelea kila shule na kuona namna ya kuwafundisha watoto masuala ya sanaa.

"Kupitia hafla hii nimeona Kaka Bonda (mtunzi wa kitabu) ana nia nzuri ya kuwainua watoto. Kwa hiyo, kupitia hiki ambacho amekifanya leo (jana) tutamwingiza katika mradi ili baadhi ya wanafunzi waliopo hapa wanufaike zaidi," alisema.

Kiongozi huyo alisema wana utaratibu wa kupita kila shule kuona namna ya kuwasaidia wanafunzi wenye vipaji, akibainisha kuwa hata jana aliona mmoja wa wanafunzi wenye vipaji, akiahidi kufika kwenye shule yake na hata kuonana na wazazi wazazi wake kwa lengo la kuendeleza kipaji hicho.

"Mimi ukiachana na kazi yangu pia kwenye maisha yangu binafsi huwa ninawasaidia watoto wenye uhitaji wa bima ya afya, kwa kuwa huo ni msaada ambao ninaufanya kwa kupenda mwenyewe, ninaomba kama kuna watoto wenye uhitaji, kuanzia mwezi wa kwanza ninaweza nikatoa msaada kwa kulipia watoto 10 au 20, nitaanza na 10, baadaye nitamalizia wengine," alisema.

Mtunzi wa kitabu hicho, Bonda, alisema kinalenga kuwafanya watoto wapende kusoma vitabu na kuijua nchi yao hususani kwenye eneo la vivutio vya utalii.

Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Ufundi Mwambao iliyoko Bagamoyo, Nakesha Dikcson alisema kitabu hicho kitawapa nafasi ya kujiongezea maarifa, kujikita kujisomea na kujiepusha na mambo yasiyofaa kwenye jamii.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Haki Miliki Tanzania, Doreen Sinare (kulia), akizungumza wakati wa uzinduzi wa kitabu cha kadogoo mtalii na kadogoo club, Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mtunzi wa kitabu hicho, Francis Bonda. **PICHA: HALFANI CHUSI.**

# Tanzania yaikabidhi Burundi kiti mkataba Ziwa Tanganyika

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imeikabidhi Burundi kiti cha uenyekiti wa mawaziri waliopo katika Mkataba wa Kikanda wa Usimamizi Endelevu wa Ukanda wa Ziwa Tanganyika na kusisitiza Kiswahili kitumike kama lugha kuu ya mawasiliano katika mikutano yote itakayofanyika.

Katika Mkutano wa 10 wa Mawaziri hao uliofanyika jana jijini Bujumbura, Burundi, baada ya Tanzania kumaliza muda wa uenyekiti uliodumu kwa kipindi cha mwaka mmoja, ilikabidhi kiti hicho.

Akizungumza wakati wa mkutano huo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo alisema Tanzania inashiriki katika shughuli zote zinazolenga kuhakikisha usimamizi endelevu wa rasilimali za ziwa hilo.

Pia alisema Tanzania imedhamiria kushirikiana na nchi wanachama ambazo ni Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Zambia katika utekelezaji wa programu za kikanda zinazolenga kulinda rasilimali za pamoja za Ziwa Tanganyika na kuboresha maisha ya watu katika bonde hilo.

Dk. Jafo alisema Ziwa Tanganyika ni rasilimali muhimu kwa wananchi takriban milioni 10 wa ukanda huo wanaolizunguka, hivyo zinahitajika juhudi za pamoja katika kulilinda.

"Waheshimiwa mawaziri, mazingira tunayoishi yanabadilika haraka sana na shughuli za binadamu zinatumia maliasili za dunia kwa kasi ya kutisha na kuharibu mifumo ikolojia.

"Inakadiriwa kuwa zaidi ya viumbe 22,000 wako hatarini kutoweka ikiwa ni pamoja na baadhi ya viumbe katika Ziwa Tanganyika," alisema.

Hivyo, alitoa wito kwa mawaziri hao kutoka nchi wanachama kuungana kwa pamoja kujadili namna bora ya kulinda Ziwa Tanganyika kwa ajili ya kizazi cha leo na kijacho huku akisisitiza umuhimu wa kuweka utaratibu wa muda mrefu wa ufadhili wa programu ya maendeleo ya Ukanda ya Ziwa Tanganyika.

Ujumbe ulioshiriki katika mkutano huo uliwajumuisha Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Dk. Switbert Makama, Mkurugenzi wa Mazingira, Dk. Andrew Komba, Ofisa Mazingira Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Deogratius Nyangu na wawakilishi wa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

# Tanzania yaishukuru Korea kutenga mkopo wa mabilioni

**Na Peter Haule,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ameishukuru Serikali ya Jamhuri ya Korea kwa kutenga dola za Marekani bilioni moja zitakazotolewa kwa njia ya mkopo nafuu kwa Tanzania kupitia Mfuko wa Shirika la Maendeleo ya Kiuchumi (EDCF) kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kipindi cha miaka mitano

Dk. Nchemba alitoa shukrani hizo jijini Dodoma juzi alipokutana na kufanya mazungumzo na waziri anayesimamia uratibu wa masuala ya Sera wa Korea, Moon-Kyu Bang aliyezuru kikazi nchini.

"Septemba mwaka 2022, Tanzania na Korea tulisaini makubaliano yatakayoiwezesha Tanzania kupata mkopo wenye riba nafuu wenye thamani ya dola za Marekani bilioni moja ambapo Tanzania itakopa mkopo huo kwa riba ya asilimia 0.01 kwa mwaka na kuulipa kwa kipindi miaka 40 ambacho kimeambatana na kipindi cha neema cha miaka 15," alisema Dk. Nchemba

Aliishukuru Korea kwa kuahidi kusaidia utekelezaji wa miradi miwili mipya ukiwamo mradi wa maji na usafi wa mazingira mkoani Iringa wa Iringa na ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Binguni-Zanzibar, ambayo italeta manufaa makubwa kwa wananchi.

Alisema wizara na serikali kwa maelekezo na mwongozo wa Rais Samia Suluhu Hassan, ipo tayari kushirikiana na timu ya Serikali ya Korea na wawakilishi wa Benki ya Exim nchini kukamilisha haraka taratibu zote za kitaalamu ili miradi hiyo itekelezwe.

Dk. Nchemba alizikaribisha kampuni za Jamhuri ya Korea kuwekeza nchini ukiwamo uwekezaji wa ubia katika miundombinu wezeshi, ikiwamo ya barabara, nishati, afya, usafiri wa majini na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Dk. Nchemba alisema Serikali ya Tanzania ina fursa nyingi za uwekezaji kwa kuwa ni lango la nchi nchingi zikiwamo za Afrika Mashariki na kusini mwa Afrika na pia ina mazingira bora ya uwekezaji na ufanyaji biashara.

Pia alibainisha ushirikiano kati ya Tanzania na Korea ni wa kirafiki na kindugu, ikizingatiwa Serikali ya Korea iliwezesha Tanzania kupata fedha za kutekeleza miradi mingi ukiwamo mradi wa ujenzi wa Daraja la Tanzanite jijini Dar es Salaam.

Waziri Ofisi ya Uratibu wa Sera wa Jamhuri ya Korea, Moon-Kyu Bang aliahidi uamuzi wa utekelezaji wa mradi wa kuboresha usambazaji maji na mazingira wa Iringa utafanyika mwishoni mwa mwaka huu na utekelezaji utaanza mara moja wakati mradi wa Hospitali ya Rufani ya Binguni, taratibu za kitaalamu zitakamilishwa ndani ya miezi sita ili utekelezwe.

Bang pia aliipongeza serikali kwa kutekeleza mradi wa kimkakati wa reli ya kisasa ambao alisema ni mkubwa na utasaidia kuinua uchumi wa nchi na nchi jirani na kuahidi kuwa atazishawishi kampuni kutoka nchini mwake kushiriki katika mradi huo kwa njia ya utaratibu wa ubia kati ya umma na sekta binafsi.

# MAISHA

DESEMBA 11, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 13

**Mavazi yaliyotamba 2022**



**MAISHA NI NYUMBA**

Faida za kitanda cha mbao




Ukurasa 12

SHEREHE



# Furahia ngozi murua

Ukurasa 14

# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA




| | |
|---|---|
| DAFTARI | PENI |
| FUNGUO | KUFULI |
| BARUA | BAHASHA |
| GOLI | MPIRA |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | T | E | N | G | A |
| | A | | | A | |
| M | K | E | | N | |
| | A | | U | D | A |
| | S | | | I | |
| T | A | M | K | A | |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
INA, MWA, SAUMU, LAANA, NYUNGU, LAWAMA

## CHEKA



Alichokifanya daktari

Nchini Marekani mama anapomuaga mtoto wake anamwambia "Usiku mwema bebi"

Uingereza mama humwambia mtoto anapotaka kulala "Lala unono bebi wangu"

Hispania mtoto anapokwenda kulala humtamkia "Usiku mwema mtoto mpendwa"

Afrika wazazi humuaga mtoto wao "umefunga milango yote haya kalale huko"

**Chemsha Bongo**

Juma na rafiki zake walikwenda kuvua samaki baharini, wakapata samaki 6 wasio na vichwa, 9 wasio na mikia 8, Je, walivua samaki wangapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Tamaa ya kutajirika haraka ilivyoharakisha wengi kufa

***KARIBU** tena msomaji wangu tujadili baadhi ya matukio tata yanayojitokeza kwenye jamii yetu. Pengine utajiuliza ni kwa nini mtu hujiua, ingawa anaonekana yupo vizuri kiuchumi na pia kiafya? Je, mwonekano wake wa nje kimwili unatudanganya?*

Nimeuliza maswali haya ili msomaji wangu upate picha ya kile ninachokwenda kujadili pamoja nawe. Mwanadamu ni mfano wa kabati lililoficha mambo mengi. Utaona mtu anapita barabarani kanawiri kiafya, amevaa vizuri lakini yale anayowaza nafsini mwake ni makubwa na magumu sana.

Tuchukue mfano wa matukio ya mtu kuchukua uamuzi wa kujiua. Yuko anayejiua kutokana na maisha magumu, umasikini unaomfanya aandamwe na madeni. Mawazo yanapofikia mwisho na suluhisho hakuna, anaamua kujilipua na kukatisha maisha.

Hawa wako wengi na tumewashuhudia ndani ya jamii yetu. Leo ninawajadili wale wenye hali nzuri kimaisha lakini ghafla wanajiua. Ukiona hivyo, ni dhahiri yako mambo yaliyojificha na yanapojitokeza hadharani, mhusika huikimbia aibu kwa kujiua!

> **“Wako marafiki utawaambia chanzo cha mafanikio yako, kisha wakafanya mbinu kukiua chanzo hicho. Matokeo yake uchumi wako unadorora au kuanguka kabisa.**

Si kwamba anapenda kuchukua uamuzi huo bali anajikuta ni lazima afanye hivyo. Maandiko ya Mungu yameweka wazi jambo hili pale ilipoandikwa. “Kwa maana lile jema nilipendalo, silitendi; bali lile baya nisilolipenda ndilo nilitendalo” (Rum.7:19). Ujumbe kwenye andiko hilo umewanasa wengi. Mahali pengine ikaandikwa, “... Hata mimi nalilipishwa kwa nguvu vitu nisivyovichukua”. (Zab.69:4).

Wako watu wanaosingiziwa kufanya jambo fulani wakati si kweli, hawahusiki. Wako pia ambao huenda kwa waganga na kupigwa chale japo hawataki. Hili ni moja ya machukizo mbele ya Mwenyezi Mungu.

Anaonya kwenye neno lake,”Msichanje chale yoyote katika nyama ya miili yenu kwa ajili ya wafu, wala msiandike alama mwilini mwenu; mimi ndimi BWANA.” Pia anasema “Usimnajisi binti yako, ili kumfanya awe kahaba; isiwe hiyo nchi kuuandama ukahaba, na nchi kujawa na uovu mkuu”.

Msomaji wangu, nimehusisha maandiko ya Mungu ili ujue ya kuwa yako maonyo anasema nasi kila siku ili tuwe salama. Nikirejea suala la kujiua ambalo limeficha mengi, kwa utafiti wangu mdogo, nimegundua yafuatayo;-

Kwanza, tamaa ya kutajirika haraka imekatisha ndoto na maisha ya watu wengi wakubwa kwa wadogo. Wapo watu wanaofanikiwa kwa juhudi za muda mrefu. Kila anayefanikiwa ipo vita alipigana hadi kufikia hapo alipo!

Alianza kidogo kidogo na mwishowe akajikuta amefanikiwa sana. Liko andiko la Mungu kwamba “Japokuwa mwanzo wako huo mdogo, lakini mwisho ungeongezeka sana”.

Wengine kwa kutojua siri ya mafanikio ya mtu mwingine, hujiingiza wazima wazima kwa tamaa nyingi, na hata kutumia njia za makato wakidhani ndio watapata upenyo mkubwa wa utajiri.

Sambamba na hilo, wanaambatana na watu wasio sahihi wenye lengo la kuwaharibia. Usipokuwa makini na marafiki, hawa ndio baadaye huwa sumu ya mafanikio yako!

Wako marafiki utawaambia chanzo cha mafanikio yako, kisha wakafanya mbinu kukiua chanzo hicho. Matokeo yake uchumi wako unadorora au kuanguka kabisa.

Wako tayari kuchunguza wafadhili na kuwalisha maneno ya uongo ili mfadhili asiendelee kukusaidia. Wahenga wakasema, “Kikulacho kipo nguoni mwako”. Moja ya neno la Mungu imeandikwa, “Adui wa mtu ni wa nyumbani mwake”.

Marafiki wengine wanaeleza siri za nyumbani mwako. Pengine unamsifia mume au mke wako. Wanapita pembeni wanamlisha mume au mkeo maneno kuhusu jambo fulani. Lengo ni kuzua mtafaruku ili ndoa iliyotulia isambaratike. Ndoa nyingi zimevunjika kwa mbinu hii!

Wengine madeni au mikopo kwa ajili ya miradi imewazidi, wanachanganyikiwa na kuamua kujilipua. Hii yote ni kutafuta utajiri wa haraka.

Mungu analijua hili ndio maana akasema, “Japokuwa mwanzo wako huo ni mdogo, lakini mwisho ungeongezeka sana”. Anatutaka tuanze na kidogo, kisha yeye atakizidisha unavyozidi kujitahidi. Usitafute mkato bali taratibu ndio mwendo.

Hii ndiyo kanuni ya Ki-Mungu. Watu wengi hawaelewi kanuni hii, wanajiingiza kutafuta utajiri wa haraka, matokeo yake wanaangamia.

Kwa mfano mwanamke anakuwa na mume wa mtu ambaye ni mashuhuri na mwenye mali nyingi. Wambeya na marafiki wa karibu wanajua wanafikisha taarifa kwa mkewe. Hapo vita lazima iinuke!

***Huko kote mtu anatafuta maisha ya juu kwa muda mfupi. Usalama upo kwenye mtaji mdogo na kumtegemea zaidi Mungu kwani yeye ni mwenye vyote! Una kisa? Ujumbe 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Ubakaji, ulawiti unaongezeka, jamii tuchukue hatua

LEO ni kilele cha siku 16 za kupinga ukatili duniani. Wadau wamekutana maeneo mbalimbali kupaza sauti dhidi ya vitendo vya ukatili ambavyo vinaumiza watu wote kwenye jamii.

Maadhimisho haya yanafanyika wakati matukio ya ulawiti na ubakaji wa watoto yanaongezeka kila uchao, kesi nyingi zinaelezwa kuishia polisi au mtuhumiwa anapopewa dhamana, familia zinakaa kuzungumza ili kuyamaliza kifamilia.

Aidha, baadhi ya vijana waendesha bodaboda wanadaiwa kuhusika na matukio hayo hasa wale wanaowabeba wanafunzi kuwapeleka shuleni, kiasi kwamba wako watoto wamefanyiwa ukatili na kuuzoea au kulazimishwa kuishi maisha ya mateso tangu wakiwa wadogo.

Kwenye shule za msingi na sekondari, matukio hayo yanaongezeka kwa watoto kufanyiwa hivyo na ndugu wa karibu ambao hulala nao wanapokaribishwa na mama, baba au mlezi anashtuka mtoto ameshaharibika.

Aidha, inadaiwa fedha inatumika kumaliza kesi hizo na wakati mwingine madawati ya jinsia yamelalamikiwa kuwa sehemu ya uharibifu, ambao sasa ni mamivu kwa jamii.

Unapokwenda maeneo ya starehe, utakutana na vijana wa kiume wa rika mbalimbali wanajiuza yaani wanaingiliwa kinyume cha maumbile na wanaume wenzao, huku wasichana wakiwa na uhusiano na wasichana au wanawake wenzao.

Vitendo hivi vinaua kizazi kwa kuwa idadi ya wanaume inaendelea kupungua kila siku, huku takwimu zilizopo zikionyesha wanaume ni wachache ikilinganishwa na wanawake, sasa linapotokea suala la ulawiti linapunguza idadi yao na kukiweka kizazi hatarini.

Inaelezwa kuwa mwanamume anapofanyiwa kitendo hicho, anatamani kuendelea kufanyiwa ndiyo maana wengi hujiuza ili kupata wa kumfanyia hivyo. Hili ni kosa kisheria na limekatazwa na kulaaniwa kwenye vitabu vitakatifu vya dini.

Utafiti mdogo uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Mashataka, ulibaini kuwa baadhi ya watuhumiwa wa makosa hayo wakiwa nje kwa dhamana, wanakimbia na wengine kuharibu ushahidi au kumalizana na wazazi ama ndugu wa mhanga wa vitendo hivyo.

Aidha, Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Happy Msimbe, hivi karibuni alisema serikali imeanza mchakato wa kufanyia marekebisho Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, wanaanza mchakato wa makosa ya ubakaji na ulawiti kuondolewa dhamana.

Baadhi ya familia zinamaliza kesi hiyo nyumbani, inapotokea mzazi mmoja anashikilia kuendelea na kesi mahakamani anaitwa na kukalishwa na ukoo, ikiwamo kutengwa kama atakubali kuendelea na kesi.

Wengi wanaokumbwa na kesi hizi wanatoka familia maskini ambazo wakati mwingine kufuatilia kesi ni usumbufu na gharama, wakati mwingine wanakutana na usumbufu mkubwa polisi na hospitali na kuamua kubaki nalo moyoni.

Wanaoteseka ni watoto na wazazi wao ambao wametendewa ukatili huo, lakini hawana pa kukimbilia kwa kuwa kila eneo hakuna msaada na mwisho matukio huendelea kutokea.

Mabadiliko ya sheria hiyo kuongeza makali ni hatua nzuri sana kwa kuwa watu wataogopa na kesi zitashughulikuwa inavyotakiwa kwa kuwa ushahidi hautaharibiwa kama inavyofanyika sasa.

Ni muhimu kulinda taifa dhidi ya ongezeko la mashoga ambao wanakuwa hivyo siyo kwa msukumo wa maumbile, bali kwa kufanyiwa ukatili na wachache ambao wananufaika au ni tamaa za mwili.

Lakini ni muhimu kuendelea kutoa elimu na kuchukua hatua mapema taarifa zinapotolewa, kuboresha madawati ya jinsia ili yasiwe kichaka cha rushwa na kuumiza watu, viongozi wa dini walio waadilifu kuendelea kuwahubiri yaliyomema waumini wao na kuwaonya kwa kutumia maandiko matakatifu juu ya vitendo hivyo.

Sheria kufanyiwa mabadiliko ni jambo jema, lakini bila kudhibiti rushwa ni sawa na bure kwa kuwa watu wataendelea kufinyanga kesi za namna hiyo, ili kupata fedha kwa waliotenda pasipo kuona uharibifu huo ipo siku utabisha hodi kwenye nyumba yake.

Kwa sasa tuna Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum, ambayo imeunda kamati mbalimbali kukabili vitendo vya ukatili, lakini ni muhimu kufuatilia hadi ngazi ya chini hasa kwenye shule za msingi na sekondari, lakini kuimarisha idara ya ustawi wa jamii, polisi na hospitali ili wafanye kazi kwa hofu ya Mungu na kuogopa kuyaharibu matukio hayo.

Lazima jamii iwe wazi kwa kusema hapana kwa vitendo vya ukatili ambao unaelekea kuwa jambo la kawaida sana,mifumo ifanye kazi vyema,kamati za kupinga ukatili kuanzia ngazi ya mtaa zitekeleze wajibu wake.

# HARUSI












Wanafunzi wa shule ya awali na msingi ya Jubilation wakiwa katika hafla ya mahafali ya kuwapongeza kwa kumaliza masomo. Mahafali hayo yaliyohudhuriwa na Mdhibiti wa Elimu mkoa, Elisafi Mgonja, yalifanyika Bunju mkoani Dar es Salaam hivi karibuni.

# MITINDO





# Mavazi yaliyotamba 2022

WAKATI 2022 ukifikia ukingoni, suala la mitindo ya mavazi lilikuwa kipaumbele kwa wanawake ambao wameonekana kung'ara.

Ndani ya mwaka nguo za aina mbalimbali zilitamba na kuonyesha ukubwa na umaridadi wake.

Baadhi ya rangi zilizotamba 2022 katika mitindo ya mavazi ni bluu,njano, kahawia, nyeusi, kijivu na dhahabu.

Wanawake bila shaka, wameweza kuonyesha kwamba wao ni vinara wa kupenda kuvaa vizuri na wengi wamejaribu kufuata mitindo ya kisasa na kujifunza kuhusu mwenendo mpya wa mtindo.

Aina ya mitindo iliyong'ara kwa mwaka huu katika majukwaa ya mitindo ni vitambaa vya asili vya metali, nguo na lurex, zilizopambwa kwa rhinestones, vitenge na hariri.

Picha zote na Pinterest

UREMBO



# Furaha ya ngozi murua

UZURI wa ngozi sio rangi tu bali ni muonekano wake kama inang'aa na yenye afya bora.

Kuna aina nyingi ya utunzaji wa ngozi na kuifanya kuwa na mwonekano mzuri, na leo nitakueleza namna ya kutunza ngozi yako kwa kutumia vitu vya jikoni.

Kwa kutumia vyakula kama kiini cha yai, machicha ya nazi, tango na limao inatosha kukupa ngozi imara.

### JINSI YA KUFANYA

Andaa maji safi yenye joto kiasi unachomudu katika ngozi yako, osha uso wako.

Kama una ngozi kavu au ya kati chukua kipande cha tango kidogo na upake yale maji yake usoni.

Kwa wenye ngozi ya mafuta unaweza kutumia kipande cha limao kwa kupaka maji yake.

Chukua pamba au kitambaa laini na kisha futa maji ya matunda kusugua taratibu usoni.

Ukimaliza chukua machicha ya nazi, sugua uso na shingo taratibu hadi uridhike umepitiwa na machicha. Kisha ondoa machicha ubaki na uso unaong'aa vyema.

Malizia kwa kuchukua kiini cha yai, inapendeza ukitumia la kienyeji au la kisasa lenye kiini cha njano iliyokolea angalau.

Paka ute mzito wa kiini cha njano uso mzima bila kusahau shingoni na nyuma ya masikio na ngozi ya masikio.



Baada ya kupaka kiini cha yai unaweza kuendelea na shughuli zako mpaka inapokauka ndipo unaondoa kwa kuivuta.

Baada ya kule kuvuta kuisha inamaanisha yai limekauka kabisa. Osha uso wako kwa maji safi maji yawe ya baridi.

### FAIDA ZAKE

Husaidia kutibu na kuikinga ngozi na chunusi, kuipa ngozi mng'ao bila kutumia kemikali za sumu, husaidia kupunguza mikunjo katika ngozi yako na hutumia gharama ndogo.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Mambo ya kuzingatia kupika pilau ya nyama

MSIMU wa Sikukuu za Krismasi na mwaka mpya umewadia, zimebaki siku chache familia zitafurahi kwa kupata chakula kizuri, mavazi na burudani.

Wapo watakaosafiri kwenda makwao kujumuika na wazazi na familia kula sikukuu na waliobaki mijini wao hukaa na familia zao na kufurahia kwa pamoja.

Katika safu yetu leo tunaangalia namna ya kufurahisha familia kwa kupika pilau la nyama.

Mara nyingi pilau linanoga likipikwa kwa nyama na viazi mviringo, wengi wanaenda mbali na kunogesha kwa kuweka njegere kwa mbali.

Wakati wa kupika pilau lako hakikisha unakuwa makini usizidishe maji na kuwa bokoboko.

Pia hakikisha unakaridia viungo kulingana na kiasi cha mchele na nyama uliyoandaa, pilau ikiwa na viungo vingi halipendezi.

Pia usisahau kuwa makini na chumvi na mafuta visizidi ikawa kero.









Bila kusahau kuwa makini chakula chako kisiungue au usipunje moto kikaiva upande watu wakala vibichi wakavimbiwa.

Kwa upande wa nyama wapo wanaopenda kukaanga, kuchoma na wengine kuoka na mvuke.

Katika kuhakikisha mnafurahia hakikisha unaandaa nyama yako mapema na uweke viungo vya kutosha kabla ya kukaanga au kuchoma ili ziive taratibu.

Kumbuka ukichelewa kuandaa kitoweo chako mapema, utafanya haraka na muda wa kula utafika watu watakula nyama mbichi au ambayo haijakolea viungo.

Pia wakati huu wa sikukuu zingatia muda wa kuandaa vyakula vyote ili watu wale kwa furaha.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Faida za kitanda cha mbao



FREMU za kitanda cha mbao kwa ajili ya kitanda ni chaguo zuri kupamba chumba na kuleta mwonekano mzuri wa ndani.

Imeelezwa fremu za mbao za kitanda ni salama zaidi kuliko za chuma kutokana na kutokuwa na ncha kali.

Hizi ni baadhi ya faida za kutumia fremu za mbao za kitanda.

**1:** Fremu za mbao za kitanda zina muonekano mzuri unaopendezesha chumba. Hasa inapotengenezwa kwa mbao zenye rangi za asili.

**2:** Zinakifanya kitanda kionekane cha kifahari na kinakipa chumba muonekano wa uhalisia, utulivu na ukamilifu.

**3:** Kitanda cha mbao ni bei nafuu ukilinganisha na ubora na uzuri wake.

**4:** Pia kitanda cha mbao kinakupa garantii ya pesa zako hadi zaidi ya miaka 30.





# Tumia pazia kupendezesha nyumba yako

PAZIA ni miongoni mwa mapambo yanayotumika sana katika kupendezesha ndani ya nyumba. Kama ilivyozoeleka, mapazia yamekuwa yakitumika kupambwa mlangoni na dirishani.

Mbali na majumbani, pazia pia hutumika sana kupambwa katika sehemu za ofisi, hotelini na sehemu nyingine nyingi.

Kadri ukuaji wa sayansi na teknolojia unavyochukua nafasi, kadhalika maisha nayo yanabadilika au kuboreka zaidi.

Kwa ujumla, mapazia katika kipindi hiki cha kasi ya ukuaji wa sayansi na tekonolojia, yamekuwa yakitengenezwa katika aina au mitindo yenye mvuto tofauti, hivyo kutoa fursa kila mtu kuchagua aina inayomfaa hasa kwa kuzingatia mandhari iliyopo ndani ya nyumba yake.

Pamoja na hayo, uchaguzi wa rangi na aina ya kitambaa kwa wale wanaopendelea kushona, nalo ni jambo muhimu linalopaswa kuzingatiwa. Wakati wa kufanya hayo yote, unapaswa kuzingatia aina ya rangi zilizoko katika nyumba yako kuanzia ukutani na vitu vingine vilivyomo ndani.

Kwa sasa pazia lina umuhimu mkubwa katika kupendezesha nyumba ndiyo maana kuna umuhimu zaidi kuzingatia kufanya uchaguzi mzuri wa pazia.

Ni vyema kutambua kuwa ubaya wa nyumba yako utatokana na namna wewe mwenyewe unavyoitengeneza nyumba na hata mvuto wake pia utategemea namna unavyochagua.

Ni jambo la aibu kuona unasifia mvuto wa nyumba ya jirani eti tu ameweka pazia nzuri, wakati na wewe mwenyewe unaweza.

Naamini kila kitu kinawezekana ukijipanga, inawezekana kabisa usitumie gharama kubwa katika kupata pazia lako zuri unalolipenda kama utajipanga na kudhamiria kuwa nalo.






Wako ambao wanaweza kutundika mapazia yao ndani ya nyumba kwa kutumia kamba za kawaida na yakapendeza lakini kama inawezekana, si vibaya kutumia fimbo maalum za kutundikia pazia.

Fimbo hizi hupatikana kwa wingi katika maduka ambayo yanauza mapazia kwa hiyo ni vyema wakati unanunua mapazia yako ukatafuta na fimbo zake.

Tafuta fimbo ambayo rangi yake inaendana na rangi iliyopo kwenye nyumba pamoja na iliyopo kwenye pazia. Epuka rangi zinazong'ara sana kwa sababu hazina utulivu, ni vyema kuchagua rangi iliyopoa.

Zingatia kuweka mapazia yako katika fimbo laini ambazo hazikwaruzi ili zisiharibu mapazia wakati unavuta kuyaweka sawa.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
USINITUMBULIE MIMACHO YAKO!
NITAWAAMBIA HUYU TOKA LIANZE KOMBE LA DUNIA ANALALA NJE
TENA BARAZANI ALAFU BILA NETI
POLISI
JUKWAANI
JANA MIKEKA YANGU YOTE ILICHANIKA KIZEMBE TU! LEO NAISHONA
HILI KARATASI LA KUBETI UTADHANI MTIHANI WA KIJELEMANI!
HIVI MANIYUU BADO YUMO?
BETI
KISTAARAB!
DUH! ZILE TIMU NAZOZIJUA ZISHANG'OKA WOLDI'KAPU... NA KUACHA KUBETI SIWEZI
HUU MZIGO SIO WAKO...
MWENYE NAO HAPA TULIPO ANAONEKANA
AFANDE HUYO SIO KONDA NI TAJIRI WA GARI 'UTAUA WATOTO!'
SIO WATOTO TU, ILE GARI INGEUA HATA ABIRIA WOTE!
AFANDE HAPO LUGHA GONGANA!
SIKU ZINAKWENDA MBIO ZINGEKUWA GARI TUNGE-HESABU EKSIDENTI KILA KUKICHA
HIZI EKSIDENTI ZINAZOTOKEA MIFUKONI KWANI HUZIONI?
KUWA SILIAZI BHANA
UNASHANGILIA NINI KAMA UME-PEWA RUKSA UKAOE WA PILI?
ASANTEEEE KOMBE LA DUNIA SIKU HIZI HATA NIRUDI SAA NGAPI SIULIZWI NILI-KUWA WAPI?
...KINYUNYIZO CHA LEO...
-KUTOBOA SIO MAFANIKIO WENGINE WAMETOBOA PUA-

# HABARI KIMATAIFA




Polisi wakilinda eneo ambalo linashukiwa kutumiwa na watu wanaotaka kuipindua serikali baada ya watu 25 wanaoshukiwa kuwa wanachama na wafuasi wa kikundi cha mrengo wa kulia kukamatwa kufuatia msako uliofanywa nchini kote Ujerumani wiki hii.
**PICHA: REUTERS**

## Marekani, Russia kubadilishana wafungwa zaidi

**MOSCOW,** RUSSIA

MAREKANI na Russia zimekubaliana kubadilishana wafungwa zaidi.

Hatua hiyo imechukuliwa siku moja baada ya nyota wa mpira wa vikapu wa nchini Marekani kuachiwa huru baada ya kubadilishwa na muuza silaha maarufu.

Brittney Griner alirejea Marekani baada ya kuwa jela kwa miezi 10 nchini Russia.

Ikulu ya White House iko chini ya shinikizo kumwachilia mwanajeshi wa zamani wa Marekani, Paul Whelan, ambaye amefungwa jela nchini Russia kwa miaka minne.

Rais Vladimir Putin alisema kubadilishana wafungwa zaidi kunawezekana na ni mfano adimu wa ushirikiano kati ya nchi hizo mbili.

Alipoulizwa katika mkutano wa kilele nchini Kyrgyzstan siku ya Ijumaa kama mabadilishano mengine ya wafungwa kati ya Marekani na Russia yanaweza kufanyika, Putin alijibu kwamba hawakatai kuendelea na kazi hiyo katika siku zijazo. Aliongeza kuwa kila kitu kinawezekana na alibainisha kuwa maafikiano yamepatikana ili kuweka mambo sawa kwa ajili ya mabadilishano.

Griner, ambaye alikamatwa Februari kwa kumiliki mafuta ya bangi katika uwanja wa ndege wa Russia, aliachiliwa baada ya kubadilishana na mlanguzi wa silaha aliyepatikana na hatia Viktor Bout, ambaye alirejeshwa nchini Russia baada ya miaka 12.

Mwanariadha huyo wa Marekani alipelekwa kufanyiwa tathmini katika Kituo cha Matibabu cha Jeshi la Brooke huko San Antonio, Texas, alipotua Marekani siku ya Ijumaa.

Haijabainika ni muda gani nyota wa Chama cha Kikapu cha Wanawake (WNBA) atasalia kwenye kituo hicho.

John Kirby wa Ikulu ya Marekani aliambia mtandao wa TV wa Marekani MSNBC Ijumaa asubuhi kwamba mshindi huyo wa medali ya dhahabu mara mbili kwenye Olimpiki alikuwa yuko sawa na afya njema.

Utawala wa Rais wa Marekani Joe Biden umekabiliwa na upinzani kwa kushindwa kumrudisha nyumbani Whelan pamoja na Griner.

Mzaliwa huyo wa Michigan alihukumiwa na mahakama ya Russia kifungo cha miaka 16 jela mwaka wa 2018.

*BBC*

## Zambia yakiri raia wake alikufa vitani Ukraine

**LUSAKA,** ZAMBIA

RUSSIA ilikuwa imempa msamaha mwanafunzi wa Zambia aliyefungwa ili ajiunge vitani nchini Ukraine.

Katika taarifa iliyotolewa na serikali ya Zambia, inaeleza msamaha huo ni kama takwa la kusamehewa na aliuawa kwenye mstari wa mbele.

Waziri wa Mambo ya Nje, Stanley Kakubo, alisema Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergey Lavrov, alimwambia kwa njia ya simu kwamba Lemekhani Nyirenda alisamehewa Agosti 23 na alijiunga na operesheni ya kijeshi badala ya kutoka jela.

Awali Russia ilitangaza kuwa Nyirenda mwenye umri wa miaka 23 aliuawa kwenye uwanja wa vita nchini Ukraine mwezi Septemba, na kusababisha Zambia kuuliza ni vipi aliishia kupigana katika vita hivyo.

"Tulifahamishwa kwamba Russia inaruhusu wafungwa kupewa fursa ya msamaha badala ya kushiriki katika operesheni maalum ya kijeshi," alisema Kakubo

Kulingana na mamlaka ya Zambia, Nyirenda alikuwa nchini Russia akisomea uhandisi wa nyuklia katika Taasisi ya Fizikia ya Uhandisi ya mjini Moscow.

Alipokea kifungo cha jela Aprili 2020, cha miaka tisa na miezi sita kwa kosa la kutumia dawa za kulevya na alikuwa akitumikia kifungo chake huko Moscow.

Waziri Kakubo alisema mwili wa Nyirenda uliwasili Moscow siku ya Ijumaa na unatarajiwa kufika Zambia leo.

Russia pia imefahamisha Zambia kwamba pesa zinazodaiwa na Nyirenda, pamoja na nyaraka zote zinazohusiana na msamaha wake, kuajiriwa na kifo, zitakabidhiwa kwa mwakilishi wa Zambia ambaye angeambatana na chombo hicho, waziri huyo alisema.

Novemba, mkuu wa kundi la mamluki la Wagner la Russia mfanyabiashara Yevgeny Prigozhin, ambaye ni mshirika wa karibu wa Rais Vladimir Putin, alikiri kuwa alimsajili Nyirenda kutoka gerezani Mzambia huyo na alikubali kwa hiari kwenda kupigana dhidi ya Ukraine.

Prigozhin alisema wakati huo kwamba Nyirenda alikufa kama shujaa na alikuwa mmoja wa watu wa kwanza kuingia kwenye eneo la adui mnamo Septemba 22.

*BBC*

## Wanasiasa feki washtumiwa kuwasajili vijana kujiunga ugaidi

**MAPUTO,** MSUMBIJI

RAIS wa Msumbiji Filipe Nyusi, amesema kuna watu wanaojifanya wanasiasa ili kuwasajili vijana katika safu ya wanamgambo wa jihadi.

Wanamgambo hao wamekuwa wakiendesha mashambulizi kaskazini mwa nchi hiyo tangu mwaka 2017.

Akizungumza katika sherehe za kuhitimu kijeshi, kiongozi huyo alisema kuwa serikali inafahamu kuhusu jambo hilo na wale watakaobainika kuhusika watafikishwa katika vyombo vya sheria.

"Watu hao, tunapowakamata, mahali pao ni jela," alisema Nyusi.

Pia alisisitiza kwamba jeshi lake lilikuwa likifanya harakati fulani dhidi ya wanamgambo hao kaskazini mwa nchi, na kufanikisha kukamatwa kwa baadhi ya wanajihadi na viongozi wao, pamoja na silaha walizotumia.

*BBC*

## Ubelgiji yaitaka Rwanda kuacha kuwasaidia waasi

**BRUSSELS,** UBELGIJI

UBELGIJI imeitolea wito nchi ya Rwanda kusitisha msaada wowote kwa waasi wa M23 wanaoendelea na mapigano katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Kauli hiyo ilitolewa baada ya uchunguzi wa Umoja wa Mataifa kubaini kuwa kundi hilo liliwaua raia 131 mwezi uliopita.

Wizara ya mambo ya nje ya Ubelgiji ilisema juzi katika taarifa yake kuwa kundi la M23 lazima lisitishe mara moja uhasama na kujiondoa katika maeneo yaliyo chini ya udhibiti wake.

Aidha, imelaani vikali mauaji ya idadi kubwa ya raia, huku ikisisitiza kuwa wahusika wa mauaji hayo hawawezi kuachwa bila kuadhibiwa.

Ubelgiji imetaka pia kukomeshwa kwa mahusiano kati ya mamlaka yoyote ya Congo na kundi la FDLR.

Mgogoro wa M23 umesababisha kuongezeka kwa mvutano kati ya Kongo na jirani yake Rwanda, ikiituhumu kuwaunga mkono waasi hao.

Rwanda imekana kutoa msaada wowote na kwa upande wake inaishutumu DRC kwa kushirikiana na waasi wa FDLR .

*DW*

MAKALA

# NECTA HILI LITAZAMENI UPYA



Na Magabilo Masambu

ELIMU ndiyo sekta mama katika nchi yoyote. Kada zingine zote zinatokana na elimu ndiyo maana baada tu ya kupata uhuru, watu wa kwanza kabisa kusomeshwa walikuwa walimu kwa sababu taifa halikuwa na wataalam wengi katika kada mbalimbali.

Kwa hiyo mwasisi wa taifa la Tanganyika na baadaye Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, alianzisha mpango wa UPE yaani 'Universal Primary Education'. Walichukuliwa vijana wenye ufaulu mzuri zaidi waliomaliza darasa la saba kuwa walimu na kutumika kufundisha wenzao.

Kutokana na umuhimu wa elimu nchini, pamekuwapo na juhudi mbalimbali za kuhakikisha sekta hiyo inakuwa bora ikiwa ni pamoja na kuhakikisha mitihani haifanyiwi udanganyifu. Katika hili, nalipongeza sana Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania (NECTA) kwa hatua ambazo limekuwa likichukua. Natambua ni kwa nia njema ya kulinda heshima na usalama wa nchi, lakini kuhakikisha taifa linapata wataalam wenye sifa na maarifa badala ya watu wenye vyeti vizuri lakini wajinga!

Hatua hizo ni pamoja na kufuta matokeo ya watahiniwa au kuzifungia kabisa shule zinazohusika katika udanganyifu wa mitihani. Natambua madhara yanayotokea ikiwa watu wataiba mitihani au kufanya udanganyifu wowote wakafaulisha, ikiwamo kupata wataalam wabovu ambao wanaweza kusababisha madhara makubwa kwa nchi.

Ikiwa daktari amepatikana kwa njia za wizi wa mitihani, maana yake anaweza kuangamiza wagonjwa wengi baadaye. Ikiwa mitihani haitadhibitiwa, tunaweza kupata viongozi wabovu wasio na maarifa mpaka ngazi ya kitaifa. Tutapata wahandisi watakaojenga magorofa mabovu ambayo yakianguka maafa yake ni makubwa. Pia tutapata mahakimu wasiojua kuhukumu kesi, hivyo watu wengi watafungwa bila hatia. Mbaya zaidi nchi ikionekana inaonyesha mitihani, maana yake wataalam wetu hawataaminika kufanya kazi katika mataifa mengine na elimu yetu kudharaulika.

Pamoja na hatua hizo nzuri za kulinda hadhi ya mitihani ili kupata wataalam mahiri, kwa mtazamo wangu, kuna jambo linahitajika kutazamwa upya. Jambo lenyewe linahusu kufutiwa matokeo kwa watahiniwa hasa wa shule za msingi na kutopewa mitihani mingine ili wafanye tena. Watoto wa shule za msingi hasa darasa la nne na la saba ni wadogo sana ambao kwa vyovyote vile, hawawezi kushawishi waonyeshwe mitihani bali wao ndio wanashawishiwa kuonyeshwa mitihani au kufanya udanganyifu.

Uhakika nilio nao ni kwamba hakuna hata mtoto mmoja anayekwenda kwa mwalimu au msimamizi na kumwambia "naomba unionyeshe au unipatie majibu ya mtihani". Wote wanapewa au kulazimishwa kupewa majibu ya mitihani. Kama ndivyo basi maana yake ukiwafutia mitihani wao halafu ukashindwa kuwapa mtihani mwingine, utakuwa umewaonea na kuwaadhibu kwa makosa yasiyo kuwa yao.

Mtoto anayebakwa huwezi ukamfunga jela pamoja na aliyembaka. Mtoto huyo ni mwathirika. Sheria zinamtambua mbakaji kama mhalifu lakini mtoto hawezi kuwa mhalifu. Maana yake ni kwamba ikitokea umefanyika udanganyifu, hatua kali zichukuliwe kwa wale waliosababisha udanganyifu huo kutokea na wala si kwa watoto ambao hawana uamuzi wa kukataa kuonyeshwa au kuhusika kwenye udanganyifu. Wanaosababisha udanganyifu huo wanazo sababu za kufanya hivyo, ikiwamo kutafuta matokeo mazuri ili shule zao zionekane zinafaulisha wapate wateja wengi. Kwa maana hiyo, watoto wanatumika kama silaha ya kufanikisha malengo ya wenye shule na viongozi wao.

Hebu fikiria mzazi ametumia gharama kubwa kumsomesha mtoto wake halafu anatokea mwalimu au mmiliki wa shule au ni ofisa fulani anayetafuta cheo kupitia matokeo ya mtihani, anafanya watoto wafutiwe matokeo! Kwa nini huyo aliyesababisha hayo yatokee asilipie gharama za watoto hao kuandaliwa na kurudia mtihani mwingine?

Kwa nini umwadhibu mtoto na mzazi wake ambao hawajahusika katika janga hilo? Mzazi anakuwa yuko nyumbani hajui kinachoendelea, mara anaambiwa mtoto wako amefutiwa matokeo. Mnataka kuwaua wazazi na shinikizo la damu? Haijakaa sawa hii hasa kwa watoto ambao bado hawana uamuzi wowote. Kwa wakubwa labda ngazi za juu, hao wanajitambua maana yake wana uamuzi wa kukataa ndiyo maana udanganyifu mkubwa unafanyika kwa hawa wa shule za msingi kwa sababu ni rahisi kuwashawishi kuliko hao wa juu.

Ni kweli kwamba udanganyifu ni uhujumu uchumi kwa sababu mitihani inaandaliwa kwa gharama kubwa lakini gharama za marudio ya mitihani zigharamiwe na wanaosababisha ili liwe fundisho kwao na si kuwaadhibu watoto. Wasitumie watoto wetu kama fimbo, washitakiwe kama wahujumu uchumi na ikithibitika wanatakiwa kufungwa hata maisha ili liwe fundisho badala ya kuwahukumu watoto wadogo ambao tunawategemea kuja kulijenga taifa letu. Madaktari wangapi, wanasheria wangapi, walimu wangapi, viongozi wangapi wanaua ndoto zao kwa kufutiwa matokeo?

Ushauri wangu kwa serikali kupitia NECTA, watoto wasiwe sehemu ya adhabu hizo bali waliosababisha hayo kutokea ndio wachukuliwe hatua. Tusiwahukumu waathirika na watuhumiwa pamoja. Inapotokea hivyo, nashauri watoto wapewe mitihani mingine na wasimamiwe vyema ili tusije kusababisha watoto wengi wa mitaani ambao wangelisoma na kufikia malengo yao.

Lazima tujiulize baada ya kuwafutia matokeo huwa wanakwenda wapi? Hata darasa la nne kurudia mwaka mzima, naona halijakaa sawa. Nashauri mara tu inapotokea pale pale, wapewe mtihani mwingine ili wasipoteze mwaka mwingine kwa uzembe wa watu wachache wasio waaminifu. Kama nitakuwa nimeeleweka vyema, basi Mwenyezi Mungu awabariki sana mwendelee kuisimamia vizuri elimu yetu nchini.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Uke wenza ukute mke mwenzio mwenye imani, la sivyo utajuta*



Na Adam Fungamwango

**Wanamuziki hao walisema Marijani alienda mbali sana kwenye maneno ya mama Fatu aliyokuwa akimjibu shoga yake, kiasi kwamba aliingiza hata mambo ya ushirikina ambayo yalitolewa na kuwekwa hayo ambayo yameandikwa na kusikika kwenye wimbo huo.**

"KWELI mama Fatu nilipokuona, sikuamini macho yangu. Nilikuwa kama niko ndotoni mama Fatu shoga yangu. Ama kweli hujafa hujaumbika, naamini ya walimwengu, jinsi umbo lako lilivyobadilika ni masikitiko kwangu. Hebu nieleze umepatwa na maswahibu gani?"

Ni swali alilokutana nalo mama Fatu mara baada ya kukutana na shoga yake njiani. Aliulizwa swali hilo kwa jinsi alivyobadilika. Amefujika, amesawajika, amekonda. Unene wote umeisha. Shepu yote imeondoka.

Maneno haya yamo kwenye wimbo uuitwao 'Uke Wenza' uliotungwa na mwamamuziki Marijani Rajabu mwanzoni mwa miaka ya 1980 akiwa na bendi ya Dar International iliyokuwa ikivuma kwa mtindo wa Super Bomboka. Mtunzi na mwimbaji huyo alikuwa akielezea juu ya kinachowapata baadhi ya wanawake wanaokwenda kuolewa na wanaume ambao tayari wana wake.

Ingawa si wote wanaopata shida, ndani ya jamii kumekuwa na shida kubwa na watu wengi wameshuhudia kadhia na madhara ya uke wenza. Inakuwa vita, patashika nguo kuchanika, wanawake kugombana wenyewe kwa wenyewe. Ukiona hadi wanamuziki wa dansi wameliweka kwenye hadhira jambo hili, ujue wameliona na si mara moja wala mara mbili.

Hata sisi wenyewe nadhani tutakuwa tumeshuhudia japo hata tukio moja la majirani au watu wanaotuhusu au kuwafahamu juu ya jambo hili la uke wenza. Hebu turudi kule njiani mama Fatu alipokutana na shoga yake, alijibu nini?

"Ooo ukewenza, kweli uke wenza una mambo, ama kweli nimeona vituko, unitizame nilivyokonda, sababu ya ukewenza. Uke wenza mimi sitaki jama sitaki, tena nimekoma hata kulisikia jina hilo sipendi. Ukewenza ni fahari kwa wanaume kwetu ni tabu. Hata mwanangu Fatu akiposwa na mwenye mke sikubali. Ukiolewa bora ukute mke mwenzio mwenye imani. Kama si hivyo nakwambia ndugu yangu utajuta, hebu nitizame mwenzio mambo yaliyonifika. Hakuna sababu ila ni sababu ya ukewenza. Ukewenza mimi hapana."

Hili ndiyo lilikuwa jibu la mama Fatu. Baadhi ya wanamuziki wa bendi ya Dar International ambao waliipigia bendi hiyo, wamesema kwenye mashairi hayo ambayo mama Fatu anajibu yalirekebishwa kwenye studio za Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD). Kamati ya kupitia maudhui ilimshauri Marijani kubadilisha baadhi ya mashairi kwani yale ya mwanzo yalikuwa makali sana na yanayochoma moyo kiasi kwamba hata wasikilizaji, hasa kinamama wangeweza kuangua vilio au kutoka na machozi.

Wanamuziki hao walisema Marijani aliienda mbali sana kwenye maneno ya mama Fatu aliyokuwa akimjibu shoga yake, kiasi kwamba aliingiza hata mambo ya ushirikina ambayo yalitolewa na kuwekwa hayo ambayo yameandikwa na kusikika kwenye wimbo huo.

Mama alikuwa akilalamika kufanyiwa mambo ya kishirikina na mke mwenzake kiasi kwamba kila anakokwenda kuangalizia kwa wataalam hawaoni ugonjwa, na wakiona wanamwambia ni mke mwenzake. Bado mama Fatu anaendelea kulalama na kutoa ushuhuda kwa yaliyomfika kutokana na kukaa ukewenza.

"Uke wenza mama, bora usikie hivyo hivyo. Uke wenza kweli hatari we mama, akinababa wanatuletea janga, fahari yao kwetu sisi matatizo."

Hayo ni kwa yaliyomfika mama Fatu. Kuna wimbo mwingine ambao ulitungwa na Juwata Jazz unaitwa 'Ete' ambao nao unamhusu mwanamke aliyekwenda kuolewa mitala, lakini yaliyomkuta, ni ya kusikitisha. Dada yake alikwenda kumpa pole na akaelezea tukio zima kama lilivyoimbwa na Msondo Ngoma.

"Ndugu yangu Ete pole kwa yaliyokufika, Ete ulipoolewa, ulimkuta mwenzako nyumbani, pendo lako kwa mume wako, lilisababisha mwenzio, kuachika bure. Nyumbani alipoondoka alikuendea kinyume yakakufika maradhi.

Mapenzi ya wake wawili, hayawezi kuwa ya kweli, yangelikuwa ya kweli Ete, yasingekufika. Tutajitahidi nduguzo maradhi yakutoke, Mola atakusaidia ndiye mwenye uwezo. Ungeyajua mama mapema, katu usingejitosa, ukewenza umekuponza Ete watesekа."

Ina maana hapa mke mkubwa alipoondoka akaenda 'kufanya yake' na Ete akaugua maradhi yasiyojulikana. Haya yapo na yanatokea kwenye jamii. Mada hii inawahusu sana akinamama. Ningependa wale wote ambao wameshawahi kupatwa na mikasa hii, kuiona jirani au kwa ndugu zao, au hata kuhadithiwa na wenzao wanitumie ujumbe kwenye namba hiyo ya chini na tutazichapisha wiki ijayo.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaji, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele. Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

# Harusi imevunjika-9

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




HIVI ni kweli kuna kijana anaitwa Said alikuwa anakutaka?" Maswali yalizidi kumiminika mdomoni mwa Jerry.

"We nani kakwambia?"

"Babu mzee Mbegu."

Zulfa akaangua kicheko cha aina yake. Ni kicheko cha umbea hivi.

"Babu naye kumbe mmbea hivi, kakwambiaje?"

"Jibu kwanza swali langu Zulfa usilikwepe." Jerry akamkazia macho huku akitabasamu.

"Huo ndiyo mzozo wenyewe. Yule kijana nilimkataa, eti alitaka anioe, kaanza kuwaambia wazazi wake, ndugu zake kabla hata hajaniambia, nikamwambia aka babu nipishe mie, aliyekwambia nina shida ya mwanaume nani? Aliyekuambia ana shida ya kuolewa nani? Ila aliumia sikufichi. Kaumia sana. Kaenda kumwambia mama yake. Yule mama naye kaniboa kweli, wacha 'anichambe', unajua nilichukia, na vitisho juu kuwa nitaona mimi na familia yangu, hata wiki haijapita nikaumwa na nyoka, ndiyo maana mama haamini kama ni kweli nyoka wa kawaida yule."

"Lakini umeponea hospitali, si ndiyo?"

"Ndiyo, ila leo Jerry una maswali kama tuko kituo cha polisi, una nini leo?"

"Nina wivu kwa Said." Akajibu huku akicheka, kicheko kilimuambukiza pia Zulfa na msichana wao wa kazi pia.

"Nimemkataa lakini, na leo niko kwako hapa, wivu awe nao nani? Wewe yeye?" Akajibu akiendelea kucheka. Kwa kipindi chote hicho alichokuwa hapo Zulfa alionekana mwenye furaha kubwa na amani ya moyo.

Akawa anashangaa ni kwa nini dada yake Vayajo alimkataa mwanaume kama Jerry na kumkimbia siku ya harusi, akisababisha ivunjike.

**********************************

Siku za kukaa kwa Jerry ziliisha. Ilikuwa miezi miwili kamili. Zulfa alikuwa mzima wa afya, huku mama sasa akimtaka binti yake akamsaidie kwa kazi mbalimbali nyumbani.

Kabla ya kuondoka Zulfa alilia mchozi. Kwa miezi mwili aliyokaa nyumbani kwa Jerry hakuwahi kuishi kwa amani, raha na kuubwaga moyo wake kama mahali hapo.

Ukichanganya na jinsi alivyokuwa akiishi na Jerry, kijana mcheshi, mstaarabu, asiye na makuu, alijihisi kama vile alikuwa ndiye mama mwenye nyumba.

Alifanya anavyotaka. Alikula anachotaka. Kuna wakati alipewa hata uhuru wa kuchagua anachotaka kula, kununua. Mbali na hayo, Jerry alikuwa akimchukua na kwenda kumtembeza sehemu mbalimbali za starehe au ambazo alikuwa hajawahi kufika Dar.

Alinunuliwa nguo mbalimbali za gharama ambazo alikuwa akizichagua mwenyewe. Kuondoka nyumbani kwa Jerry na kurudi Kibaha kwake ilikuwa kama kutoka peponi kwenda Jehanam.

Hakutegemea tena kama anaweza tena kuishi maisha yale ya raha aliyoishi nayo miezi miwili, ambayo alikuwa hajawahi kuyapata tangu aanze kujitambua.

Si kwao Kibaha wala kwa shangazi yake Morogoro alikowahi kuishi kwa raha na amani kama pale.

"Naondoka tu sina jinsi Jerry. Lakini nitayakumbuka maisha yote ambayo nimeishi hapa. Nimeishi hapa roho yangu nyeupe.

Hakuna sehemu niliyoishi kwa amani kama hii. Nitaukumbuka upendo wako na kila kitu ambacho umenifanyia. Wewe ni mwanaume mwema sana. Yoyote anayekufanyia ubaya, au aliyekufanyia ubaya, yeye ndiyo mbaya. Nilikuwa sikufahamu sasa nimekufahamu vema. Ahsante sana. Mungu akubariki milele."

Jerry alimtazama Zulfa. Akatabasamu halafu akapanua mdomo wake.

"Ahsante, nashukuru sana, lakini hata wewe ni mwanamke mwenye upendo. Tumeishi hapa kama mtu na shemeji yake, lakini ulikuwa na upendo wa hali ya juu. Ulikuwa ni rafiki yangu ambaye nilikuwa nikirejea nyumbani sisikii maumivu wala uchovu wa kazi kwa sababu nilikuwa na mtu ambaye nikirejea napiga naye stori ambazo ni mimi na wewe tu ndiyo tulikuwa tunazipenda. Wengine wanaziona kama za kitoto mno. Lakini hazichoshi na hazileti msongo wa mawazo. Hata mimi nitaathirika sana na wewe kuondoka hapa. Kifupi nimekuzoea na nilipenda tuendelee kuwa wote."

Zulfa alirejea Kibaha si tu kwamba alikuwa amepona, lakini amenawiri, akiwa na mavazi mengi mazuri na ya kisasa ambayo yalimfanya kuonewa kijicho cha wasichana wenzake.

Kwa bahati mbaya alirejea peke yake. Hakusindikizwa na Jerry. Alikuwa amepata safari fupi ya kikazi. Awali aliomba kwanza arejee ndiyo amrudishe. Lakini ndiyo wakati mama alimhitaji zaidi Zulfa arudi nyumbani.

Alirejea siku mbili baada ya dada yake Vayajo naye alirejea, ikiwa ni miezi sita baada ya kutoroka kwenye sherehe ya harusi yake. Tukio ambalo lilizua gumzo kubwa si kijiji kwao Msangani, bali Kibaha nzima na maeneo ya jirani.

> **Hakutaka kuelezea lolote lile lililotokea. Kila kitu kilibaki ni siri yake. Hata wazazi wake ambao walitaka kuuliza ilikuwaje akafanya kitendo kile, jibu lake lilikuwa moja tu. "Nyinyi niacheni tu. Sina hata hamu ya kujibu hilo."**

Hakutaka kuelezea lolote lile lililotokea. Kila kitu kilibaki ni siri yake. Hata wazazi wake ambao walitaka kuuliza ilikuwaje akafanya kitendo kile, jibu lake lilikuwa moja tu.

"Nyinyi niacheni tu. Sina hata hamu ya kujibu hilo."

Wazazi wakaamua wakamuacha. Wakampokea kwa sababu ni binti yao. Watamtupia nani? Tikiti baya shambani mwako. Ingawa aliwatia aibu ya mwaka, lakini watafanyaje?

Kingine ambacho walifanya wasimsakame sana binti yao ni kutopata upinzani kutoka kwa Jerry na familia yake. Walilia. Wakahuzunika, wakaondoka. Kikubwa zaidi hadi leo hii Jerry amekuwa kama ndugu yao. Amekuwa akifika kijijini hapo kwa mambo mbalimbali.

Mara ya mwisho kumchukua Zulfa kwa ajili ya kumtibia, akigharamia kila kitu. Na akakaa na binti yao miezi miwili. Mwisho cha muhimu zaidi wakajua labda mambo yanaweza kumalizwa kidiplomasia na Vayajo akachukuliwa na Jerry. Ni kwa sababu amerudi nyumbani na pia bado wana mahusiano mazuri na muoaji.

Vayajo alikuwa anafahamu kila kitu kilichokuwa kikitendeka kwao tangu aondoke. Alikuwa anazipata habari kutoka kwa rafiki yake Nasma, au Naa kama ambavyo kijijini hapo walikuwa wanapendelea kumwita.

Alipotoroka alibadilisha namba ya simu. Lakini mara chache alikuwa akiirudisha ile namba ya awali, anampigia Naa na kumuulizia habari za kijijini hapo na nyumbani kwao, akiridhika, anang'oa laini na kuirudishia ile mpya. Ya zamani inakuwa haipatikani tena.

Taarifa za ndugu yake kuumwa na nyoka, kulazwa pia alikuwa nazo ingawa hakuja. Taarifa za kuchukuliwa na kukaa kwa aliyemkimbia kabla ya ndoa pia zilikuwa mikononi mwake.

**INAENDELEA JUMAPILI**



# CELINE DION AFICHUA UGONJWA UNAOMTESA

MKONGWE wa muziki wa kimahaba, Celine Dion amefichua hali ya afya yake na kueleza anasumbuliwa na ugonjwa nadra wa neva wa Stiff Person Syndrome (SPS) ambao hauna tiba.

Amesema ugonjwa huo unajumuisha mfumo wa kinga kushambulia chembe hai nyeupe.

Mwimbaji huyo wa Kifaransa mwenye asili ya Canada, amewaambia wafuasi wake milioni 5.2 kupitia ukurasa wake wa Instagram, kuwa hali hiyo inamfanya misuli yake kutetemeka bila kudhibitiwa.

Amesema hali hiyo inamfanya kuwa na ugumu wa kutembea na kuimba.

Kauli yake hiyo inamaanisha kuwa hataweza kufanya maonyesho yaliyopangwa nchini Uingereza na Ulaya mwaka ujao.

"Nimekuwa nikikabiliana na matatizo ya afya yangu kwa muda mrefu," Dion amesema.

Ameongeza "Imekuwa vigumu kwangu kukabiliana na changamoto hizi na kuzungumza juu ya kila kitu ambacho nimekuwa nikipitia,"

Akaendelea kuwaambia mashabiki wake "Hivi majuzi niligunduliwa kuwa na ugonjwa wa nadra sana wa neva unaoitwa 'stiff person syndrome' ambao huathiri mtu mmoja kati ya milioni moja.

"Wakati bado tunajifunza juu ya hali hii adimu, sasa tunajua ugonjwa huu ndio umekuwa ukisababisha magonjwa yote ya misuli au mishipa kuanza kutetemeka ambao nimekuwa nao."

"Kwa bahati mbaya, mishtuko hii ya misuli huathiri kila nyanja ya maisha yangu ya kila siku, wakati mwingine husababisha ugumu wakati ninapotembea na kutoniruhusu kutumia sauti yangu kuimba jinsi nilivyozoea," akamalizia kusema.





# Davido kufunga kombe la dunia

STAA wa muziki wa Afropop kutoka Nigeria, Davido anatarajiwa kutumbuiza katika tamasha la kufunga mashindano ya kombe la dunia nchini Qatar.

Msanii huyo akifanikiwa kutumbuiza, itakuwa mara ya kwanza kwake kuonekana hadharani tangu kifo cha mwanawe Ifeanyi aliyefariki wiki kadhaa zilizopita.

Habari za Davido kutumbuiza katika sherehe za kufunga kombe la dunia zilifichuliwa na rafiki yake ambaye ni mfanyibiashara kutoka Hong Kong kwa jina Stephen Hung.

Kumbuka kwamba nyota huyo wa muziki hapo awali alipewa kadi ya kutumbuiza kwa wimbo wa Kombe la Dunia kwenye sherehe ya ufunguzi, lakini hakuweza kufanya hivyo baada ya kifo cha mtoto wake.

Hung aliandika: "Nimefurahi sana kaka yangu @davido alithibitisha kuwa atatumbuiza kwenye sherehe za kufunga Kombe la Dunia Qatar. Siwezi kungoja kumuona huko.".



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### VLAHOVIC KUTUA ARSENAL

KLABU ya Arsenal inaweza kufufua nia yao ya kumnunua mshambuliaji wa Juventus na Serbia, Dusan Vlahovic, 22, kufuatia jeraha la goti alilopata Gabriel Jesus, 25, alipokuwa akiichezea Brazil Kombe la Dunia. ***(Calciomercatoweb)***

#### FELIX KUBADILISHWA

JUVENTUS watakuwa tayari kumtoa Dusan Vlahovic kwa Atletico Madrid katika mpango wa kubadilishana kiungo wa Ureno, Joao Felix, 23. ***(Calciomercatoweb)***

#### SANE AWINDWA

ARSENAL ni chaguo kwa winga wa Bayern Munich na Ujerumani, Leroy Sane, 26, ikiwa hatasaini nyongeza ya mkataba mwanzoni mwa msimu ujao. ***(Bild)***

#### ENRIQUE ATAKIWA ATLETICO

KLABU ya Atletico Madrid inaweza kumchukua kocha wa zamani wa Hispania, Luis Enrique, 52, kama mrithi Diego Simeone. ***(AS)***

#### DALOT KUONGEZEWA

KLABU ya Manchester United itafungua mazungumzo ya mkataba mpya na Diogo Dalot, 23 atakaporejea kutoka Kombe la Dunia kufuatia beki huyo wa kulia kuonyesha uthabiti kwa Ureno. ***(Fabrizio Romano)***

#### MUANI ANAFUATILIWA

MSHAMBULIAJI wa Fiorentina, Randal Kolo Muani, 24, ambaye thamani yake ni pauni milioni 26 anafuatiliwa na Liverpool, Tottenham Hotspur na Atletico Madrid. ***(Fichajes)***

#### KLICH ATAKIWA DC UNITED

KIUNGO wa kati wa Poland, Mateusz Klich, 32, yuko kwenye mazungumzo na klabu ya DC United, inayofundishwa na Wayne Rooney, kuhusu uwezekano wa kuhama kutoka Leeds United. ***(MLS Soccer)***

#### MCKENNIE KUUZWA

KLABU ya Juventus iko tayari kumuuza Weston McKennie, 24, na wamemthaminisha kwa pauni milioni 26, huku Chelsea na Tottenham Hotspur zikihusishwa na kiungo huyo wa Marekani. ***(Calciomercato via Metro)***

#### CONTE ALIMTAKA BASTONI

MLINZI wa Inter Milan na Italia, Alessandro Bastoni, 23, amesema kocha zamani, Antonio Conte alijaribu kumsajili Tottenham Hotspur msimu wa joto. ***(Corriere dello Sport via 90 min)***

#### KARIUS MKATABA MPYA

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe anataka kumuongezea mkataba golikipa wa Ujerumani, Loris Karius mwenye umri wa miaka 29.***(Mail)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# PELE AMTAKA NEYMAR KUENDELEA BRAZIL

**SAO PAULO,** Brazil

### ●●● Ni baada ya nyota huyo kuonesha kuwa anaweza kustaafu baada ya kombe la Dunia...

PELE amempongeza Neymar kwa kufikia rekodi yake ya muda mrefu ya ufungaji mabao akiwa na Brazil na akamtaka fowadi huyo "kuendelea kututia moyo" huku kukiwa na maswali kuhusu mustakabali wake wa kimataifa.

**Neymar alifunga bao lake la 77 kwa Brazil katikati ya muda wa nyongeza na kufungua ukurasa wa mabao katika robo fainali ya Kombe la Dunia Ijumaa dhidi ya Croatia kwenye Uwanja wa Education City.**

Hata hivyo, Bruno Petkovic alisawazisha dakika ya 117 na Croatia wakaishangaza Brazil kwa mabao 4-2 kupitia mikwaju ya penalti na kutinga nusu fainali, ambapo sasa watakutana na Argentina Jumanne.

Nyota wa Paris Saint-Germain, Neymar alipendekeza baada ya mechi hiyo anaweza kuwa amecheza mchezo wake wa mwisho kwa Selecao hao, ingawa hajafanya uamuzi rasmi.

Katika kile ambacho kilikuwa tukio chungu kwa kijana huyo mwenye umri wa miaka 30, Pele - ambaye amelazwa hospitalini akiwa na ugonjwa - aliingia kwenye mitandao ya kijamii kumpongeza.

"Nilikuona ukikua, nilikushangilia kila siku na hatimaye naweza kukupongeza kwa kusawazisha idadi ya mabao yangu na timu ya taifa ya Brazil," aliandika Pele kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Sote wawili tunajua hii ni zaidi ya idadi. Jukumu letu kubwa kama wanamichezo ni kuhamasisha.

"Kuwatia moyo wenzetu wa leo, vizazi vijavyo na zaidi ya yote, kuhamasisha kila mtu anayependa mchezo wetu.

"Kwa bahati mbaya, siku hii si ya furaha zaidi kwetu, lakini daima utakuwa chanzo cha msukumo ambao wengi wanatamani kuwa.

"Nimejifunza kuwa kadiri muda unavyosonga ndivyo urithi wetu unavyoongezeka. Rekodi yangu iliwekwa karibu miaka 50 iliyopita, na hakuna aliyeweza kuikaribia hadi sasa.

"Umefanikiwa, kijana. Hii inaongeza ukubwa wa mafanikio yako. Hata hivyo, unajua, kama mimi, hakuna idadi kubwa zaidi ya furaha ya kuiwakilisha nchi yetu.

"Nina umri wa miaka 82, na baada ya muda huu wote, natumaini nimekuhimiza kwa njia fulani kufikia hapa. "Zaidi ya hayo, ninatumaini kuwa mafanikio yako yataenea kwa mamilioni ya watu wanaokufuata kupinga kile kinachoonekana kuwa ngumu."

SportPesa | LIVE IN PLA


MECHI KALI
WATFORD
VERSUS
HULL CITY
1 | 1.62
X | 3.61
2 | 5.34

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ARSENAL WATAFUTA MRITHI WA JESUS



**LONDON,** England

ARSENAL wameripotiwa kuwa wanaongoza kwenye mbio za kumnasa mshambuliaji wa Juventus, Dusan Vlahovic baada ya kuumia kwa Gabriel Jesus.

Vlahovic mwenye umri wa miaka 22 alinunuliwa kutoka Fiorentina kwa Euro milioni 70 Januari mwaka huu, na alianza kampeni ya sasa ya Serie A akiwa na kiwango kizuri, akiwa na mabao sita na asisti katika mechi 10 alizoanza.

Alikosa michezo minne ya mwisho ya ligi ya Juventus kuelekea mapumziko ya Kombe la Dunia kutokana na jeraha, na alishindwa kuwa na athari kubwa kwa Serbia kwenye kombe la dunia nchini Qatar, akifunga bao moja.

Ingawa bado ana misimu mingine kwenye mkataba wake, misukosuko ya nyuma ya pazia ya Juventus inaweza kuwafanya Arsenal kumpata kirahisi.

Ripoti hiyo ina maana kwamba Vlahovic atauzwa tu ikiwa ni lazima kufanya hivyo, na, muhimu zaidi, kwamba haitakuwa hadi mwisho wa msimu.

Huku Jesus akitarajiwa kukaa nje miezi mitatu baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti, Arsenal wanahitaji kupata mshambuliaji mwingine.



## *Messi: Maradona 'anatusukuma kutoka mbinguni'*

**DOHA,** Qatar

KUFANIKIWA kwa Argentina kutinga nusu fainali ya Kombe la Dunia kulimfanya Lionel Messi kusema Diego Maradona "anatusukuma kutoka mbinguni".

Argentina haijashinda michuano hiyo tangu Maradona alipoongoza ushindi wao wa pili mwaka 1986.

Nahodha wa Albiceleste, Messi kwa muda mrefu amekuwa akilinganishwa na Maradonna, huku uchezaji wake nchini Qatar ukihimiza matumaini ya kutwaa taji la tatu lililokuwa likisubiriwa kwa muda mrefu.

Messi alitoa pasi ya bao kwa Nahuel Molina dhidi ya Uholanzi katika robo fainali ya Ijumaa, kisha akaiongezea timu yake bao la pili kwa mkwaju wa penalti.

Lakini Argentina walipata hofu kubwa kwani mabao mawili ya Wout Weghorst yalipelekea sare hiyo kuwa ya penalti.

Emiliano Martinez aliokoa mipira miwili, na kuiruhusu Argentina kupenya kabla ya kusherehekea uwanjani mbele ya mashabiki wao - huku Maradona akiwa maarufu katika mawazo yao.

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# TSHALA MUANA AFARIKI DUNIA

**KINSHASA,** DR Congo

MWIMBAJI nguli wa muziki wa rhumba, Elisabeth Tshala Muana amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 64.

**Habari za kifo chake zilithibitishwa na mume wake, Claude Mashala mapema jana asubuhi.**

"Mapema asubuhi ya leo (jana) Bwana mwema amefanya uamuzi wa kumuita tena Tshala Muana. Mola mwema atukuzwe kwa nyakati zote njema alizotujalia hapa duniani. Kwaheri Mamu kutoka kwangu," alinukuliwa Mashala na BBC.

Juni mwaka 2020, kulitokea uvumi kwamba amefariki, lakini badala yake akalazwa hospitalini baada ya kuugua ugonjwa wa kiharusi.

Tshala Muana Muidikay aliyezaliwa Mei 13 mwaka 1958, alikuwa mwandishi na mpiga densi wa Kikongo kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Anachukuliwa kuwa "Malkia wa Mutuashi", muziki wa kitamaduni na dansi kutoka eneo lake la asili la Kasai, katikati mwa nchi ya DR Congo.

Mara nyingi watu humuita "Mamu National", mama wa taifa.

Anajulikana kwa nyimbo kadhaa kama vile "Karibu Yangu", "Malu", "Tshianza", "Tshibola" na zingine nyingi. Amefanya ziara nyingi nje ya nchi, ameshinda tuzo kadhaa na amerekodi zaidi ya albamu 20.

## Simba kushusha vyuma dirisha dogo

INATOKA UK. 24

"Unajua tulipata mafanikio makubwa miaka ya karibuni tu hapa, kwa hiyo ni ngumu kuendelea kuwa nayo pale kwa miaka yote ni lazima uyumbe na kuna wakati unaweza kushuka kwa ghafla, muda si mrefu tunarejea kwenye maisha yetu ya ubora," alisema.

Ahmed pia aliwazungumzia wachezaji ambao wamo midomoni mwa wanachama na mashabiki wa Simba hasa kuelekea kwenye dirisha dogo la usajili, Manzoki na Ntibazonkiza kuwa kama mambo yakienda sana wanaweza kuvaa uzi mwekundu na mweupe.

"Kama kila kitu kitakuwa sawa basi Manzoki atakuja, ni aina ya mashambuliaji ambaye kila timu Afrika ingependa kuwa naye, anajua mpira na anajua kufunga, akija tutajivunia kuwa naye.

"Kuhusu Ntibazonkiza ana takwimu nzuri, ana 'asisst' nyingi na anafunga mabao, kiwango chake kinajieleza, kama ataonekana anastahili na mapendekezo yatamuangukia Saido, basi hakuna wasiwasi atajiunga na Simba, ni mchezaji mkubwa anastahili kuichezea Simba," alisema Meneja Habari huyo.



Tshala Muana akiwajibika jukwaani enzi za uhai wake. **PICHA: MAKTABA**

## *Yanga kazi moja tu kwa Kurugenzi leo*

INATOKA UK. 24

Kaze alisema hawataidharau Kurugenzi kwa sababu hadi kufikia hatua hiyo ni timu nzuri na inauwezo kwa kupata matokeo katika uwanja wowote.

Nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, alisema wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanawatoa wapinzani wao na kusonga mbele.

"Tunahitaji kutetea taji hili la FA, kufika mbali ni lazima kuanza kufanya vizuri kuanzia mchezo huo, kikubwa ni kuwaomba mashabiki wajae uwanjani kutupa sapoti," alisema Mwamnyeto.

Mechi zingine ambazo zitachezwa leo ni KMC FC itakayocheza na Tunduru Korosho katika dimba la Uhuru, Dar es Salaam saa 10.00 alasiri.

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 11/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1445 | Boluspor vs Bandirmaspor | 2.17 | 3.16 | 3.11 |
| 14:00 | 2041 | Athletic Bilbao B vs Atletico Baleares | 2.62 | 3.11 | 2.52 |
| 14:00 | 3261 | Atletico Madrid B vs CD Guadalajara | 1.81 | 3.25 | 4.18 |
| 14:00 | 3289 | Racing Santander B vs Real Oviedo B | 1.89 | 3.17 | 3.90 |
| 14:00 | 4202 | Tiddim Road Athlectic Club vs Neroca FC | 2.13 | 3.25 | 3.40 |
| 14:15 | 5783 | Willem II Tilburg vs NAC Breda | 1.86 | 3.60 | 3.70 |
| 14:30 | 4757 | Cagliari vs Perugia | 1.91 | 3.17 | 4.16 |
| 15:00 | 4176 | Tabor Sezana vs Olimpija Ljubljana | 4.86 | 3.64 | 1.61 |
| 15:30 | 5912 | Universitatea Cluj vs UTA Arad | 2.48 | 2.98 | 2.93 |
| 16:00 | 1042 | Genclerbirligi vs Erzurum BB | 2.73 | 3.26 | 2.35 |
| 16:00 | 3337 | UD Ibiza Eivissa vs Malaga | 2.20 | 2.87 | 3.61 |
| 16:00 | 4597 | QPR vs Burnley | 2.97 | 3.31 | 2.27 |
| 16:00 | 4877 | Gillingham vs Bradford City | 3.19 | 3.09 | 2.26 |
| 16:30 | 1891 | De Graafschap vs FC Eindhoven | 2.10 | 3.44 | 3.15 |
| 16:30 | 2465 | Telstar vs Den Bosch | 1.96 | 3.60 | 3.35 |
| 16:30 | 2685 | Roda Kerkrade vs Heracles Almelo | 2.56 | 3.45 | 2.47 |
| 16:30 | 3374 | VVV Venlo vs Maastricht | 1.96 | 3.65 | 3.31 |
| 16:30 | 3890 | Almere City vs ADO Den Haag | 1.84 | 3.65 | 3.75 |
| 16:30 | 3969 | FC Oss vs Dordrecht | 2.02 | 3.66 | 3.16 |
| 16:30 | 4948 | Thailand vs Myanmar | 1.17 | 7.08 | 15.16 |
| 16:30 | 5536 | Jong Ajax vs Jong Utrecht | 1.48 | 4.51 | 5.30 |
| 17:00 | 1209 | Benevento vs Cittadella | 2.22 | 2.97 | 3.42 |
| 17:00 | 3918 | Maribor vs ND Gorica | 1.22 | 5.44 | 10.70 |
| 17:00 | 4263 | Spal vs Palermo | 2.53 | 2.97 | 2.87 |
| 17:00 | 4437 | Ascoli vs Genoa | 3.01 | 2.91 | 2.47 |
| 17:30 | 2250 | Penybont vs Airbus UK Broughton | 1.14 | 6.63 | 13.66 |
| 17:30 | 2550 | Caernarfon Town vs The New Saints | 10.71 | 6.62 | 1.17 |
| 17:30 | 3654 | Pontypridd Town vs Bala Town | 4.48 | 3.99 | 1.60 |
| 17:30 | 3741 | Newtown AFC vs Haverfordwest | 2.08 | 3.41 | 3.07 |
| 18:00 | 1764 | Oldham vs Torquay | 1.96 | 3.50 | 3.45 |
| 18:00 | 1989 | Watford vs Hull City | 1.62 | 3.61 | 5.34 |
| 18:00 | 2284 | Omonia Nicosia vs Akritas Chlorakas | 1.41 | 4.60 | 7.00 |
| 18:00 | 4248 | Talaea El Gaish vs Al Masry Club | 3.45 | 2.95 | 2.26 |
| 18:15 | 3524 | Sporting Gijon vs FC Cartagena | 2.33 | 2.87 | 3.32 |
| 18:30 | 3315 | Botosani vs CFR Cluj | 4.75 | 3.46 | 1.72 |
| 19:00 | 1574 | Altinordu vs Bodrumspor | 3.07 | 3.41 | 2.08 |
| 19:00 | 3401 | Alcorcon vs Cordoba | 2.33 | 3.05 | 2.91 |
| 19:30 | 1036 | Zamora CF vs RS Gimnastica de Torrelavega | 1.78 | 3.22 | 4.38 |
| 19:30 | 5973 | NK Radomlje vs NK Celje | 3.99 | 3.60 | 1.75 |
| 20:00 | 2055 | Szeged vs MTK Budapest | 3.15 | 3.40 | 2.05 |
| 20:00 | 4640 | Bari vs Modena | 1.91 | 3.28 | 3.98 |
| 20:00 | 4853 | AEL Limassol vs Aris Limassol | 3.29 | 3.29 | 2.16 |
| 20:15 | 1615 | Marino Luanco vs CD Laredo | 1.99 | 3.06 | 3.69 |
| 20:30 | 1970 | Eibar vs Real Oviedo | 1.81 | 2.99 | 5.18 |
| 20:30 | 3208 | Granada vs Burgos | 2.03 | 2.88 | 4.16 |
| 21:30 | 1961 | Chindia Targoviste vs Steaua Bucuresti | 3.32 | 3.27 | 2.12 |
| 22:00 | 2710 | Sporting Braga vs Pacos Ferreira | 1.21 | 6.42 | 11.04 |
| 22:30 | 1477 | Frosinone vs Pisa | 1.90 | 3.17 | 4.17 |
| 23:00 | 3914 | Las Palmas UD vs Albacete Balompie | 1.67 | 3.27 | 5.75 |
| 23:00 | 5224 | Racing Santander vs Mirandes | 2.17 | 2.88 | 3.68 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Desemba 11, 2022
Nipashe



Tshala Muana afariki dunia UKURASA 23



Wachezaji wa Yanga wakiwa mazoezini. **PICHA: YANGA**

## Simba kushusha vyuma dirisha dogo

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema itasajili wachezaji wachache lakini wenye uwezo mkubwa kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chao, huku straika Cesar Manzoki na kiungo mshambuliaji wa Geita Gold, Saido Ntibazonkiza wakitajwa kuwa huenda wakajiunga na timu hiyo.

Meneja habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally amesema wanakoelekea ni kugumu hivyo ni lazima walete watu wenye uwezo mkubwa wenye kuleta ushindani, kwani wanaelekea kwenye mzunguko wa pili wa Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tunakokwenda ni kugumu kuliko tulikotoka kwa hiyo ni lazima tulete watu kweli, watu wenye ushindani," alisema Ally.

"Kwenye hili dirisha dogo tutafanya maboresho kidogo kwa ajili ya kuongeza nguvu na chachu kwenye michuano iliyo mbele yetu, ligi kuu inaelekea duru ya pili ambayo ni ngumu zaidi kwa hiyo ni lazima uwe na kikosi imara. Tunaelekea pia kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, lazima uwe na kikosi cha watu ambao watakuwezesha kushindana kwa hiyo tutafanya maboresho kidogo kuelekea kwenye ubora tunaoutaka," alisema Ahmed.

Alisema pamoja na kwamba kikosi chao ni kizuri, lakini hakijafika ule ubora ambao wanachama na mashabiki wa Simba wanaufahamu na kuuhitaji.

"Kikosi hakijafika kile kiwango ambacho tunakitaka. Wenyewe wanachama, na mashabiki wa Simba wanaifahamu timu yao, wanakifahamu kikosi chao. Simba tuna timu yetu ambayo kila mwanasimba akikaa anaifahamu. Ukisikia Mwanasimba anasema timu yetu bado hairidhishi hailinganishi na timu nyingine hapa Tanzania, anailinganisha Simba na Simba yenyewe."

"Tulikuwa na kikosi ambacho hata ukiambiwa upange kikosi, utapanga kwa kubahatisha kwa sababu wote wana uwezo wa kucheza kikosi cha kwanza. Niseme kweli kuwa bado hatujafikia Simba ile ambayo wenyewe tunaitaka, lakini hakuna mashaka, tunaitengeneza timu yetu.

INAENDELEA UK. 23

# Yanga kazi moja kwa Kurugenzi leo

### ...Ni katika mchezo wa kombe la FA, kocha asema hautakuwa mchezo rahisi na...

**Na Saada Akida**

HAITAKUWA nyepesi, ni kauli ya Yanga kuelekea mchezo wao wa leo wa Kombe la Shirikisho, FA, hatua ya pili, dhidi ya Kurugenzi FC.

**Yanga inatupa karata yake ya kusaka ushindi dhidi ya timu hiyo kutoka Simiyu katika uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam saa 1:00 usiku.**

Yanga inashuka dimbani ikiwa ndio bingwa mtetezi wa kombe hilo baada ya kumfunga Coastal Union katika fainali uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha msimu uliopita.

Katika mchezo wa leo, Yanga itawakosa nyota wake watatu ambao ni Abdultwalib Mshery, Farid Mussa na Salum Abubakari 'Sure Boy', wanaotarajiwa kuwa nje ya uwanja kwa wiki kadhaa kutokana na majeruhi.

Katika hali hiyo kikosi cha Yanga kitakuwa na mabadiliko madogo ili kuhakikisha wanafanikiwa kuvuna ushindi dhidi ya Kurugenzi yenye maskani yake mkoani Simiyu.

Kwa upande wa Kurugenzi msimu wa 2021 ilitwaa ubingwa wa mkoa wa Simiyu na kushiriki Ligi ya Mabingwa wa Mikoa na kupanda Daraja la Pili.

Katika ushiriki wake msimu uliopita haikuweza kupanda kucheza Championship na sasa inapambana kusaka nafasi hiyo, mechi ilizocheza timu hiyo hadi sasa imeshinda tatu, sare mbili na kupoteza mara mbili na kuwa nafasi ya tano kwenye msimamo wa Kundi B wakiwa na pointi 11.

Hii ni mara ya kwanza kukutana kwa timu hizo na mshindi atafuzu hatua ya 32 ya michuano hiyo.

Yanga kupitia kocha msaidizi, Cedric Kaze imesema mechi hiyo haitakuwa rahisi kwa sababu wanaenda kukutana na timu ambayo hawaifahamu.

Kaze alisema licha ya timu hiyo kucheza ligi daraja la chini lakini hawajapata mteremko wowote kwa sababu timu za aina hizo mara nyingi zinakuwa ngumu kwa timu kubwa kupata matokeo.

"Tumefanya maandalizi ya kutosha, mechi sio rahisi kama inavyofikiriwa kwa sababu tunahitaji kupata matokeo ya ushindi tusonge mbele halikadhalika na wapinzani wetu, wao wataka ushindi pamoja na kuona wanaifunga timu kubwa," alisema kocha huyo.

Alisema wachezaji wako tayari kwa ajili ya kuhakikisha wanafanya vizuri na kupambana kupata matokeo mazuri bila kujali wanakutana na timu ya aina gani.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >